SportPesa
TZS. 804,667,160
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



'**Wazazi** epukeni kulaza watoto na watu wazima chumba kimoja'

UKURASA 8




UKURASA 22


# Nipashe

Jumatatu Januari 3, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579814

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper


# Mfumo dume, ubaguzi upuuzwe nchini – CCM

●●● **Yasema** watu wa aina hiyo ni hatari... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO


UKURASA WA 3
**MAKAZI HOLELA 35,000 KURASIMISHWA**
CHUO cha Ardhi Morogoro (ARIMO) kinatarajiwa kurasimisha makazi...

UKURASA WA 4
**WAZIRI ATAKA TANESCO KUJITATHMINI**
NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana na Ajira, Patrobas...

UKURASA WA 9
**UUAJI TEMBO KAMA USHUJAA WADHIBITIWA**
IMANI ya kabila la Waberbaig mkoani Manyara ya kila mwisho wa mwaka...


## Majaliwa akemea fitina, uroho wa madaraka

UKURASA 2



Moja ya nyumba 21 za wakazi wa Halmashauri ya Mlimba Wilaya ya Kilombero mkoani Morogoro ikiwa imeezuliwa na upepo ulioambatana na mvua kubwa iliyonyesha mwishoni mwa wiki. **PICHA: IDDA MUSHI**

## Nyumba zaezuliwa, zaidi ya 100 wakosa makazi

UKURASA 8



Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store

**MICHEZO** **PABLO KUGEUKIA DARASA PENALTI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na mkewe Mary (kulia), wakiagana na viongozi wa Wilaya ya Ruangwa kabla ya kuondoka wilayani humo kuelekea Songea kwa ziara mkoani Ruvuma. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Mfumo dume, ubaguzi upuuzwe - CCM

**Na Beatrice Shayo**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimesema kila kinachofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan, kina baraka za chama huku kikionya na kutaka kupuuzwa kwa hoja dhaifu za mfumo dume na ubaguzi.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Shaka Hamdu Shaka, alitoa onyo hilo jana wakati wa dua maalumu ya kumwombea Rais Samia iliyofanyika Magomeni, jijini Dar es Salaam.

Alisema kutokana na kasi ya utendaji wa Rais Samia ni wazi kuwa amewanyima hoja wanaompinga na sasa wameanza kuibua hoja zilizojaa mfumo dume na ubaguzi na kutaka watu hao wapuuzwe kwa kuwa ni hatari kwa taifa.

"CCM ipo madhubuti, Tanzania ipo imara na salama kwenye mikono ya Rais Samia na niwapongeze Watanzania kila kunapoibuka jambo kubwa linalogusa maslahi ya taifa wameungana kulinda heshima na maslahi ya nchi kwanza, huu ndiyo utaifa na uzalendo wa kweli," alisema Shaka.

"Ni wazi Rais Samia ataendelea kufanya mema kwa Watanzania yatakayosaidia kuleta maendeleo endelevu katika kusukuma mbele mafanikio ya kiuchumi, kijamii na kisiasa nchini," aliongeza Shaka.

Kwa mujibu wa Shaka, kazi zote zinazofanywa na Rais Samia katika kuwatumikia Watanzania ni utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi na chama kimezibariki.

Kadhalika, CCM imesema Rais Samia amedhamiria kufungua uchumi wa nchi na mtu mmoja mmoja, jambo ambalo limejidhihirisha kwa vitendo kupitia utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Alisema Rais Samia ameimarisha na kuboresha mazingira ya biashara nchini hali iliyochochea biashara nyingi kurejea, ikiashiria kuwa hali ya uwekezaji nchini sasa ni rafiki na wezeshi.

"Rais Samia ameondoa urasimu katika usajili wa biashara na ameondoa ukusanyaji kodi kwa mabavu. Hali hii imewafanya Watanzania kuona fahari ya kulipa kodi kwa hiari," alisema Shaka.

Alisema kuimarishwa kwa hali ya ufanyaji biashara kumechochea upatikanaji wa manufaa ikiwamo kuongezeka kwa makusanyo ya mapato ya serikali.

Shaka alisema Rais Samia ameonyesha ubunifu na uwezo mkubwa wa kupanga vipaumbele na rasilimali za serikali katika kuhakikisha kila shilingi inayokusanywa, inayozalishwa au inayopatikana inakwenda kuongeza thamani kwenye maendeleo ya nchi na maisha ya Watanzania.

"Ndiyo sababu tumejionea miradi mikubwa ya kimkakati ikiendelea, miradi ya ujenzi wa barabara na madaraja ikiendelea, miradi ya maji nayo ikiendelea tena kwa kasi nzuri.

"Kazi zote hizi na nyinginezo anazofanya Rais Samia ni utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025, hivyo chama kinaridhishwa na kasi yake na kinamuunga mkono kwa asilimia 100," alisema Shaka.

**MAOMBI**

Alipongeza kufanyika kwa dua hiyo kwa kuwa Rais Samia anafanya kazi kubwa ambayo inahitaji msaada wa maombi ili afanikiwe.

"Ninawashukuru sana viongozi wetu wa dini mliotuongozea dua na maombi kwa ajili ya Rais wetu. Urais wa nchi ni jukumu kubwa na zito, linalolohitaji hekima, busara, afya njema, uadilifu, uzalendo na hofu ya Mungu ili kuweza kubeba matumaini na matarajio ya wananchi kwa kuwaongoza kwa haki na usawa pamoja na kuheshimu utawala wa sheria, dua na sala ni muhimu ili aweze kumaliza utumishi wake kwa mafanikio na salama."

Naye Mbunge wa Kinondoni, Abbas Tarimba, aliwataka wananchi kuendelea kumuunga mkono Rais Samia kwa kuwa ni kiongozi aliyejipambanua kupigania maslahi ya wote.

"Tumwombee Rais Samia, ni kiongozi wa mfano kitendo cha kwenda kukopa fedha nje na kuwaeleza Watanzania amekipata kiasi gani na zinatumikaje huku zikigawanywa na kuleta manufaa kwa nchi nzima, ni cha mfano na kinapaswa kupongezwa," alisisitiza.

# Majaliwa akemea fitina, uroho madaraka

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewaonya watu wanaotafuta madaraka kwa kutengeneza fitina na mbinu nyingine chafu za kuharibia wengine kwenye uongozi, kutambua kuwa uongozi unapangwa na Mungu.

Akizungumza hivi karibuni jimboni kwake Ruangwa, mkoani Lindi, Waziri Mkuu alisema madaraka yoyote yanatolewa na Mungu ambaye amepanga nani atakuwa nani katika kipindi gani na kwamba hata mtu akilazimisha kutaka nafasi hatafanikiwa kama Mungu hajakubali.

"Na wala usitumie njia yoyote kumwaathiri mwenzako ili apate madhara eti atoke hapo wewe uende, nani amekwambia utakwenda, nani amezungumza na Mungu? Tuache tabia hiyo na tuache viongozi wafanyekazi yao ya kuwahudumia Watanzania na si kuwatengenezea migogoro kila siku, tena mingine ya kusingizia," alisema.

Alisema kila nafasi imetengenezwa na Mungu na kila anayekwenda kuongoza Mungu ndiye kasema utakuwa pale.

"Utatumia mihela mingi itapotea, utakwenda na mambo ya giza hutakwenda, Mungu amesema huyu ni huyu. Tuheshimu walioko kwenye nafasi ya kuwatumikia Watanzania wafanye kazi yao kwa weledi, jukumu letu Watanzania kila mmoja kwa dhehebu lake ni kuliombea taifa, kuombea viongozi awajaze busara za kuona nini Watanzania wanahitaji ili waendelee kutumikiwa."

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, "Uongozi wa sekta yoyote unaongozwa na Mungu, unaweza kupambana sana unataka ukae ukakuta hukai anakaa mwingine, utaanza kuwaathiri wanaokaa hapo kwasababu unataka na Mungu hataki, lazima tujue madaraka yote yanatolewa na Mungu."

HABARI KITAIFA

## RC ahamasisha kilimo mkataba

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKUU wa Mkoa Ruvuma, Brigedia Wilbert Ibuge, amewataka wakulima kufuata mpango wa utekelezaji wa shughuli za kilimo kwa pamoja na cha mkataba katika msimu wa kilimo kwa mwaka 2021/2022.

Akizungumza wakati wa kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC), kilichofanyika Manispaa ya Songea, aliyataja mazao hayo kuwa ni alizeti, soya na ufuta ambayo yanalimwa kwa wingi mkoani humo na yamekuwa na soko baada ya wanunuzi kuyafuata wenyewe.

Alisema kuwa lengo la mpango huo ni kuwaongezea tija na kipato zaidi wakulima kupitia mazao yanayouzwa kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani.

Kwa mujibu wa Mkuu huyo wa Mkoa, hadi sasa umetambua maeneo yanayofaa kwa kilimo cha pamoja cha jumla ya ekari 48,343.35 zilizoko katika halmashauri zote za mkoa wa Ruvuma, na kwamba maandalizi ya utekelezaji na mpango huo yanaendelea miongoni mwake ikiwa ni kugawa mbegu za alizeti kwa wakulima ambayo inauzwa kwa bei nafuu.

Alifafanua kuwa mbegu za soya zinatarajiwa kufikishwa katika Mkoa wa Ruvuma wakati wowote kuanzia wiki ijayo na kwa msimu wa mwaka 2021/2022 mpango huo unalenga kulima mashamba jumla ya ekari 12,204 kati ya hizo 5,279 zitalimwa ufuta, ekari 3,590 soya na ekari 3,435 zitalimwa alizeti.

Kwa mujibu wa Brigedia Ibuge, utekelezaji wa aina hiyo ya kilimo utaleta tija zaidi katika mfumo wa utekelezaji wa stakabadhi ghalani kwa kuwa wana taarifa kuwa wakulima kupitia mfumo huo wataweza kuzalisha kwa kiwango kikubwa mazao hayo na kuwaletea manufaa makubwa wakulima kwa kuwapatia fedha zitakazoweza kuwaboreshea maisha yao ya kila siku.

"Eneo la stakabadhi ghalani Mkoa wa Ruvuma utaendelea kusimamia kama ambavyo walivyofanya katika msimu uliopita wa kilimo na hapa nieleze kidogo mafanikio ya mfumo wa stakabadhi ghalani kwa mwaka msimu wa kilimo uliopita wa mwaka 2020/2021 kwenye zao la ufuta peke yake jumla ya kilo 8,326,686 za ufuta ziliuzwa kati ya bei ya Sh. 1,998 na 2,393 kwa kilo moja ambapo tumefikia kupata fedha kwenye eneo hili jumla ya Sh. bil 17.2,"alisema.

Aidha, aliwahimiza wananchi wa mkoa huo kuona umuhimu wa kujikita zaidi katika kilimo cha mazao ya alizeti, soya na ufuta ambayo yameonekana kuleta tija katika maeneo mengi yanayolimwa mazao hayo.

Kwa upande wake, Mbunge wa Jimbo la Nyasa, Injinia Stela Manyanya, aliomba serikali ya mkoa huo pamoja na wadau mbalimbali kuona umuhimu wa kuchangia fedha kwa ajili ya kuwajengea uzio wanafunzi wa shule ya msingi ya elimu muhimu ya Luhila ili waweze kuepukana na matatizo yanayoweza kutokea katika maeneo wanayo ishi kwani ni ya bweni lakini haina uzio.

# Makazi holela 35,000 kurasimishwa

**Na Munir Shemweta,** MBEYA

CHUO cha Ardhi Morogoro (ARIMO) kinatarajiwa kurasimisha makazi holela 35,000 katika Mji Mdogo wa Mbalizi, mkoani Mbeya.

Kazi hiyo ni utekelezaji wa programu ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi, ambayo ni zaidi ya Sh. bilioni 50 kwa ajili ya kuzikopesha halmashauri 55 nchini.

Akizungumza jijini Mbeya mwishoni mwa wiki, Mkuu wa Chuo cha Ardhi Morogoro, Huruma Lugalla alisema, kiasi cha Sh. bilioni 1.2 kitatumika kwenye kazi hiyo na kwamba lengo ni kukamilisha ifikapo Aprili, 2022.

"Malengo yetu kazi hii ikamilike katikati ya mwezi Aprili mwaka huu kwa kukamilisha kupanga na kupima viwanja vyote 35,000 pengine nusu ya ya viwanja, hivyo viwe vimefanyiwa utaratibu wa kumilikishwa," alisema.

Kwa mujibu wa Mkuu huyo wa Chuo cha Ardhi Morogoro, iwapo kazi hiyo itakamilika kwa wakati watakuwa wameisaidia serikali na wananchi wa Mbalizi kupata maeneo yaliyopangwa na kupimwa sambamba na kuwa na umiliki wa uhakika.

Lugalla aliongeza kuwa mikakati ya chuo hicho ni kukamilisha miradi yake yote ya urasimishaji kwa wakati sambamba na kuwasaidia wananchi kupata hati ili wazitumie kwa shughuli za maendeleo huku serikali nayo ikipata mapato kupitia kodi ya pango la ardhi.

"Pamoja na kazi ya hapa Mbalizi, lakini tumefanya kazi pia katika Jiji la Arusha, Kata ya Muriet ambako tumepima viwanja 20,222 na pia tumefanya Dar es Salaam Kata ya Kivule tulikopima viwanja 30,140 na zoezi linaloendelea ni kupata uidhinishaji kwa baadhi ya viwanja kutoka ofisi ya ardhi mkoa," alisema Lugala.

Kwa upande wake, mratibu wa mradi huo wa urasimishaji makazi holela eneo la Mbalizi, Manyama Majogollo alisema timu ya wataalamu imeshafika Mbalizi kwa matayarisho ya awali kabla ya kuanza kazi rasmi.

"Kazi hizi za awali zikikamilika tunatarajia kuingia uwandani Januari 10, mwaka 2022 na kwa hivi sasa pamoja na maandalizi mengine pia tumeanza kuandaa vigingi na timu imesambaa kila eneo kuhakikisha tunaratibu vizuri maana nina imani tukianza vizuri tutamaliza vizuri," alisema Majogolo.



Wateja wakichagua matikiti maji katika Soko la Vetenari jijini Dar es Salaam jana, tikiti moja liliuzwa kwa Sh. 2,000 hadi Sh. 5,000 kwa bei ya jumla. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# PM avutiwa kasi utekelezaji miradi maendeleo

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewapongeza wakuu wote wa mikoa na wilaya nchini kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kusimamia miradi ya maendeleo na hasa ujenzi wa madarasa.

"Kupitia kwako Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa na wakuu wa wilaya walioko hapa, nitoe pongezi kwa wakuu wengine wa mikoa na wilaya kwa kazi nzuri ya kusimamia miradi ya maendeleo. Hii ni pamoja na usimamizi wa fedha, uratibu wa matumizi ya fedha hizo na usimamizi wa kuhakikisha miradi inakuwa ya viwango," amesema.

Alitoa pongezi hizo jana wakati akizungumza na viongozi wa chama na serikali wa Mkoa wa Ruvuma kwenye Uwanja wa Ndege wa Ruhuwiko, wilayani Songea, baada ya kupokea taarifa ya mkoa huo. Alisema amefanya ziara kwenye mikoa ya Mbeya, Lindi, Dodoma, Dar es Salaam na sasa yuko Ruvuma na kujionea kazi nzuri iliyofanyika.

Aliagiza ifikapo Januari 5, usafi ufanyike kwenye madarasa yaliyojengwa ili yakabidhiwe kwa wakuu wa shule.

"Ari ya usimamizi wa ujenzi iliyoonyeshwa katika miradi hii, ikifanyika kwenye miradi mingine yote, ni lazima nchi hii itafika mbali. Tunatambua katika miradi mikubwa kama hii hapakosi changamoto, lakini kuna wengine ambao wamefanya kazi nzuri hadi kubakiza fedha."

Aliwataka wasimamie miradi iliyosalia ya afya, maji na ujenzi wa barabara (TARURA) kwa mtindo huohuo. Alimwahidi Mwenyekiti wa CCM wa mkoa huo, Oddo Mwisho, kwa niaba ya wenzake, kwamba serikali itasimamia vizuri miradi mingine kama ilivyosimamia miradi hii ya maendeleo.

Wakati huohuo, Waziri Mkuu amesema sio sahihi kuiita miradi inayotekelezwa hivi sasa kuwa ni ya UVIKO-19, bali ni miradi ya maendeleo ya kitaifa ambayo inatokana na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu aliwataka wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya nchini wawahimize wananchi kwenye maeneo yao watunze akiba ya chakula walichonacho na wapunguze kukiuza. "Wakuu wa mikoa na wilaya kaeni na wananchi na kuwasisitiza wahifadhi chakula na wapunguze kuuza ili kujiwekea akiba. Kama kuna mbegu za muda mfupi ni vema wahimizwe kuzitumia ili waweze kuzalisha chakula kingine ndani ya muda mfupi. Tuendelee kuwatia moyo wananchi wetu, tushirikiane pia na viongozi wa dini ili tumuombe Mungu atushushie mvua za kutusaidia kupata mazao," alisema.

Ili kurejesha uoto wa asili ndani ya miaka mitatu hadi minne ijayo, aliwataka wawahimize wananchi kupanda miti pindi mvua zikianza. "Tukirejesha misitu midogo midogo, hali ya unyevu na uchepechepe itarejea haraka. Tunapaswa pia kukemea tabia ya kukata miti hovyo," amesisitiza.

Mapema, Mkuu wa Mkoa huo, Brigedia Jenerali (Balozi) Wilbert Ibuge, alimweleza Waziri Mkuu kuwa mkoa huo ulipokea Sh. bilioni 10.24 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 500 na mabweni matatu kwa ajili ya shule zenye mahitaji maalum.

"Kwa sasa, ujenzi wa madarasa yote 500 umekamilika kwa asilimia 100 na ujenzi wa mabweni haya matatu unaendelea vizuri isipokuwa wamefikia hatua ya maboma. Tunaahidi kuwa yatakamilika kabla shule hazijafunguliwa," alisema.

Alisema kwenye sekta ya afya, walipokea Sh. bilioni 22.75 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya kwenye tarafa 11 ambazo hazikuwa na vituo vya afya kabisa.



Ofisa Mifugo Kata ya Migoli, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Charles Koti (kushoto), akimpatia dawa ya kuzuia magonjwa mmoja wa punda katika kijiji cha Mbweleli, ikiwa ni mpango wa serikali wa kuwapatia matibabu wanyama kwa kushirikiana na Taasisi ya Inades Formation Tanzania mwishoni mwa wiki. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Waziri ataka TANESCO kujitathmini

**Na Mwandishi Wetu,** SHINYANGA

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana na Ajira, Patrobas Katambi, amelitaka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mkoani Shinyanga, kujitathmini utendaji kazi wao, ambapo limekuwa likilalamikiwa kwa utoaji wa huduma mbovu kwa wananchi.

Katambi ambaye ni Mbunge wa Shinyanga Mjini, alibainisha hayo juzi kwenye kikao cha kusikiliza taarifa za utendaji kazi kwa mwaka uliopita, kutoka katika taasisi mbalimbali za serikali.

Alisema amepokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi, kuhusu utendaji kazi usioridhisha wa shirika hilo, ikiwamo kushindwa kuwaunganishia umeme kwa wakati licha ya kulipia huduma hiyo, pamoja na kutofanya marekebisho ya ufungaji mita nzima baada ya kuzitoa mbovu, na badala yake wanatembea nazo kwenye magari.

"Malalamiko ya kukatikakatika kwa umeme hilo tatizo nalifahamu ni la nchi nzima, ambapo kunafanyika maboresho ya vifaa, lakini hili la kuchelewa kuunganisha huduma za umeme wananchi limekuwa sugu, naombeni mjitathmini na kama mnashindwa kufanya kazi, ni mwambie Waziri wa Nishati atutafutie watu sahihi," alisema Katambi.

"Taarifa zenu pia za kufungia watu huduma ya umeme zinachanganya, juzi nilipofanya mkutano wa hadhara Kaimu Meneja wako, alisema mna wateja 900 wa kufungia umeme na kila siku mnafungia wateja 40, wewe meneja unasema mnawateja 3,000 hapa mkweli nani sasa," alihoji Katambi.

Vile vile, alilitaka shirika hilo kuongeza ufanisi wa utendaji wao kazi, na sio kusukumwa au hadi kupewa agizo na viongozi, badala yake wafanye kazi kwa kufuata miongozo na kuhudumia wananchi bila ya kujali matabaka.

Naye Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko, alidai shirika hilo ni kikwazo mjini humo, huduma zao haziridhishi na sio wa kweli, hata taarifa zao wanazozitoa kwenye kikao cha Naibu Waziri Katambi zinatofautiana na zilizowasilishwa kwenye kikao cha Baraza la Madiwani, na kuonyesha jinsi walivyo wababaishaji.

Diwani wa Kizumbi, Lubeni Kitinya, awali alidai baadhi ya watumishi wanaendekeza rushwa hasa ya Sh. 30,000 ndipo watoe huduma, mtu ana zaidi ya miezi sita tangu alipie huduma ya kufungiwa umeme, lakini hajafungiwa, na mita ikiharibika wanatembea nayo kwenye magari hadi wapewe pesa.

Naye Diwani wa Kambarage, Hassani Mwendapole, alilitaka shirika hilo wafanyakazi wanapokuwa katika majukumu yao washirikiane na viongozi wa serikali wa maeneo husika na kwamba kwenye mtaa wake wa Mwasele kwa sasa kuna mgogoro mkubwa, wananchi wa mtaa mwingine waliomba umeme, lakini wamepelekewa mtaa ambao haukuomba.

"Naomba nitoe ushauri kwa TANESCO, mnapokuwa mnatekeleza miradi yenu, tushirikisheni viongozi wa maeneo husika, kama zinavyofanya taasisi zingine, sasa hivi ninapozungumza mmenitengenezea mgogoro mkubwa sana, na kama nina uwezo zile nguvu za umeme mlizoweka kwenye ule mtaa ambapo wananchi hawakuomba ningezitoa," alisema Mwendapole.

Kwa upande wake, Meneja wa Shirika la TANESCO mkoani Shinyanga, Mhandisi Grace Ntungi, alisema maelekezo na ushauri waliopewa wataufanyia kazi, na awali akiwasilisha taarifa yake, alitaja miradi ya usambazaji umeme ambayo wanaitekeleza mkoani humo kwa mwaka wa fedha (2021/2022), kuwa ni miradi 74 yenye thamani ya Sh. bilioni 2.8.

# Aonya wanaotisha wakulima wa pamba

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amewaonya maofisa watendaji wa vijiji na maofisa watendaji wa kata Wilaya ya Maswa, Mkoa wa Simiyu, kuacha mara moja tabia ya kuwatisha kuwakamata na kuwaweka mahabusu wakulima wa pamba waliochanganya zao la pamba na mahindi katika shamba moja.

Akizungumza kwa nyakati tofauti katika mikutano ya hadhara iliyofanyika mwishoni mwa wiki kwenye vijiji vya Gumali na Masela, alisema hali hiyo imezua taharuki kwa wakulima wa wilaya hiyo.

Waziri Ndaki ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Maswa Magharibi, alisema serikali ya mkoa wa Simiyu kupitia kwa Mkuu wa Mkoa, David Kafulila, imeshatoa tamko la wakulima waliochanganya mazao hayo kwenye shamba moja kutosumbuliwa wala kung'olewa mahindi na kukamatwa kutokana na hali ya hewa ya mkoa huo kwa mwaka huu kuelezwa kutokuwa na mvua za kutosha.

Alisema hali hiyo imezua taharuki kwa wakulima wa jimbo hilo na wilaya hiyo kwa ujumla na kumfanya kuamua kufanya ziara ya ghafla kwenye vijiji hivyo, ili kusikia malalamiko hayo kutoka kwa wananchi.

Alisema alipata taarifa kuwa wapo baadhi wa watendaji wanaopita kwenye nyumba za wakulima kuwatisha kuwakamata na kuwaomba rushwa ya fedha.

Kwa mujibu wa Waziri Ndaki, watendaji wote watakaobainika kutenda vitendo hivyo kwa wakulima hata kuwa na urafiki nao, atapambana kuhakikisha hatua za kinidhamu na kisheria zinachukuliwa dhidi yao.

Alisema wananchi wamekuwa wakitishwa na kutakiwa kutoa kiasi cha fedha kati ya Sh. 50,000 hadi Sh. 100,000 ili wasiweze kukamatwa kwa kuchanganya mazao hayo katika shamba moja na kuomba kupatiwa taarifa za watendaji wa serikali wenye tabia hiyo ili aweze kuwashughulikia.

# Watanzania watakiwa kuombea amani

**Na Steven William,** MUHEZA

WATANZANIA wilayani Muheza, mkoani Tanga, wametakiwa kuiombea amani nchi, ili kusitokee wanaoweza kuleta machafuko.

Ombi hilo limetolewa juzi na Mchungaji Msaidizi wa Kanisa la Anglikana Mtaa wa Madaba, wilayani hapa, Arthur Mhando.

Alisema kuwa Watanzania wana wajibu mkubwa kuiombea amani nchi inapoingia mwaka mpya wa 2022, ili kusitokee machafuko ambayo yatavunja amani.

Mhando alisema amani ndiyo msingi mkubwa katika taifa la Tanzania kwa maana hiyo hakuna budi kuombea amani nchi na viongozi wao wakuu.

Alisema pia kila mmoja anapaswa kumuomba Mungu atokomeze janga la ugonjwa hatari wa UVIKO-19 huku akiwataka waumini kujitokeza kwenda kupata chanjo hiyo ambayo alisema haina madhara.

Mchungaji Mkuu wa Kanisa la Anglikana Mtaa wa Madaba, Paul Luhinga, aliwaasa waumini kuacha kufanya mambo maovu katika kipindi cha Mwaka Mpya na badala yake watende mema ya kumpendeza Mungu.

Kwa upande wake, Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Usharika wa Muheza, Jonathan Mwamboza, alisema Watanzania wanatakiwa kuwa watenda mema ya kumpendeza Mungu katika kipindi cha mwaka mpya.

Mchungaji Msaidizi KKKT Usharika wa Muheza, Crispus Kanju, alisema Watanzania wanatakiwa kuupokea mwaka kwa kutunza amani ya nchi ambayo ni tunu.

Kwa upande wake, Padri wa Kanisa Kuu la Katoliki, wilayani Muheza, Martine Kihiyo, aliwataka waumini wa kanisa hilo kuupokea mwaka mpya kwa upendo na kufanya mema hapa dunia ya kumpendeza Mungu.

# NEMC yaafiki viwango uhifadhi majitaka Barrick

**Na Faustine Feliciane**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limesema limeridhishwa na hatua zilizochukuliwa na kampuni ya uchimbaji madini ya dhahabu ya Barrick North Mara kupunguza majitaka kutoka lita milioni nane hadi chini ya 800,000.

Septemba mwaka 2019, wakati Barrick wanachukua umiliki wa mgodi huo uliokuwa chini ya Kampuni ya Acacia, NEMC iliitaka Barrick kupunguza hifadhi ya majitaka kwenye bwawa la TSF ifikapo Desemba 31, mwaka 2021.

Akizungumza na gazeti hili, Mkurugenzi wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alithibitisha kuwa kampuni hiyo imefikia lengo walilopewa miaka mitatu iliyopita ambavyo ni viwango vya hifadhi ya mazingira.

"Ni kweli wamefikia lengo tulilokuwa tumewapa wakati wanauchukua mgodi, lile bwawa lilikuwa lina hifadhi majitaka mengi sana, sasa wataalamu wetu waliwapa lengo kuhakikisha ndani ya miaka mitatu tangu wameanza kumiliki mgodi kushusha kiwango cha uhifadhi majitaka kwenye bwawa lao angalau kuwa chini ya lita 800,000 na wamefanikiwa kufikia hilo lengo," alifafanua Dk. Gwamaka.

Awali, akizungumza na waandishi wa habari hivi karibuni ndani ya mgodi wa Barrick North Mara wilayani Tarime, Meneja Mkuu wa mgodi huo, Apolinaly Lyambiko, alisema mgodi huo umetumia Sh. bilioni 149.7 kujenga bwawa hilo na kiwanda cha kusafisha majitaka, na kwamba kumesaidia kupunguza kiwango cha maji kwenye bwawa hilo.

"Kwa sasa majitaka tunayokusanya kutoka mgodini yamefikia lita chini ya 800,000, na haya maji tunayasafisha kwenye kiwanda chetu kipya na kupata majisafi ambayo tunayarejesha kwenye matumizi ya kawaida yakiwa majisafi na salama," alisema Lyambiko.

Alisema kuwa maji hayo wanayagawa kwa wanavijiji wanaozunguka mgodi huo kwa ajili ya kupunguza kero ya uhaba wa maji safi na salama. "Kwa sasa tunasambaza maji kwenye magari, lakini tayari tumeshapanga kuanzia mwaka huu tutaanza ujenzi wa mabomba, ili kusambaza maji kwa wananchi wa vijiji vinne, mchakato huu umeshaanza," alisema Lyambiko.

Kwa mujibu wa Meneja huyo, vijiji vinne vya Matongo, Nyabichune, Nyangoto na Mjikati wilayani Tarime vinauhitaji wa maji lita 2,000,000 kwa siku na kiwanda kipya cha kusafisha maji walichokijenga kina uwezo wa kuzalisha zaidi ya kiwango hicho cha maji kwa siku.

"Tutagawa hayo maji vijijini kupitia mabomba tutakayoyasambaza kuanzia mwaka huu (Januari 2022), majisafi tunayozalisha tuna uwezo wa kugawa kwenye vijiji hivyo na mengine kubaki kwa ajili ya matumizi ya mgodini," alibainisha.

Kwa upande wao, Wenyeviti wa vijiji vya Matongo, Dausi Itembe na Nyamaganya Marwa wa kijiji cha Komarera wakizungumza kwa niaba ya wananchi wao, walisema ushirikiano mzuri wanaoupata kutoka kwa uongozi wa mgodi huo umesaidia kumaliza changamoto walizokuwanazo.

"Kwa sasa tunaishi vizuri sana, mgodi umetatua migogoro tuliyokuwa nayo huko nyuma, kulikuwa na kero ya majitaka, lakini kwa sasa hakuna na tumekuwa tukipata majisafi kutoka mgodini," alisema Itembe.

"Kwa kweli tunashukuru, tangu kuingia kwa mgodi huu mwaka 2019 zile kero zote wamezifanyia kazi na tunaishi vizuri, vijana wetu wanapata ajira kwenye mgodi na kusaidia kutunza familia," alisema Marwa.

Migodi huo wa North Mara na Bulyanhuru wilayani Kahama Mkoa wa Shinyanga inamilikiwa na kuendeshwa kwa pamoja kati ya kampuni ya Barrick Gold Mine na serikali kupitia kampuni ya Twiga Minerals Corporation waliochukua umiliki kutoka kampuni ya Acacia Septemba mwaka 2019.

## Mwinyi kuzindua matembezi ya Mapinduzi leo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, leo anatarajiwa kuzindua matembezi ya hiari yaliyoandaliwa na Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) ikiwa ni shamrashamra za miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Gymkhana mjini hapa, Naibu Katibu Mkuu wa UVCCM, Mussa Haji Mussa, alisema matembezi hayo yatazinduliwa leo kijiji cha Konde Wilaya ya Micheweni, Pemba.

Alisema yatawashirikisha vijana kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar na Januari 7, mwaka huu, yatafungwa na Rais Samia Suluhu Hassan katika viwanja vya Makombeni, mkoani Pemba.

Alisema lengo la matembezi hayo ni kuunga mkono harakati za waasisi wa Mapinduzi walioipatia uhuru nchi.

"Wazee wetu walifanya kazi ya kutupatia uhuru ambao leo hapa sisi vijana ni matunda ya Mapinduzi kwa sababu mapinduzi haikuwa kazi rahisi wapo waliopoteza uhai wao, lakini walipigania ili kutupatia uhuru," alisisitiza.

Alisema vijana watayaenzi Mapinduzi hayo kwa matembezi hayo ambayo yataambatana na shughuli mbalimbali ikiwamo ujenzi wa shule, vituo vya afya na zingine za kijamii.

Aliwataka vijana mbalimbali kujitokeza kwa wingi katika matembezi hayo ambayo kaulimbiu ya mwaka huu ni 'Uchumi wa bluu ni fursa yetu vijana kuitumia ipasavyo'.

Alisema bado vijana hawana uelewa kuhusu dhana ya uchumi wa bluu na kwamba fursa hiyo wakiitumia ipasavyo wataondokana na tatizo la kutokuwa na ajira.



Ofisa Afya Kata ya Kigamboni, Maimuna Mwaya, akimchoma sindano ya chanjo ya UVIKO-19 mmoja wa wananchi waliofika kupata chanjo hiyo katika Uwanja wa Swala, wilayani Kigamboni, mwishoni mwa wiki. Kulia ni Diwani wa kata hiyo, Dotto Msawa. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## TPHPA yatoa elimu matumizi sahihi viuatilifu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAKULIMA wa pamba, mahindi na mpunga, kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa, wamepewa mafunzo ya kutumia viuatilifu kwa usahihi ili kuua wadudu mashambani na kupata mavuno mengi.

Mtafiti Mwandamizi kutoka Mamlaka ya Afya ya Mimea na Udhibiti wa Viuatilifu Tanzania (TPHPA) ambayo zamani ilijulikana (TPRI), Ramadhani Kilewa, alisema wametoa mafunzo hayo kwa wakulima zaidi ya 80 Kanda ya Ziwa, ili wakawe mabalozi kwa wenzao na kukuza sekta ya kilimo.

Alisema kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa wakulima kuwa viuatilifu vya siku hivi havifanyi kazi na kushindwa kuua wadudu mashambani, lakini imegundulika kuwa hawajui kuvitumia kwa usahihi, na kusababisha mazao yao kuendelea kushambuliwa na kukosa mavuno mengi. "Mafunzo haya ya matumizi sahihi ya viuatilifu tumeyatoa kwa wakulima zaidi ya 80 kutoka Kanda ya Ziwa, ukiwamo mkoa wa Simiyu, Geita, Mwanza na wenyeji Shinyanga, ambayo yatakwenda kubadilisha dhana iliyojengeka kuwa viuatilifu vya siku hizi ni feki, ambapo wakivitumia kama tulivyowafundisha watapata mavuno mengi," alisema Kilewa. Kwa upande wake Katibu Tawala Mkoa wa Shinyanga, Zuwena Omary, akizungumza kwenye mafunzo hayo, aliwataka wakulima hao wakayatumie vizuri mafunzo waliyopata na kufundisha wenzao matumizi sahihi ya viuatilifu, ili wapate mavuno mengi na kukua kiuchumi.

Alitoa tahadhari kwa wafanyabiashara wanaosambaza au kuuza pembejeo za kilimo, wasiuze viuatilifu feki ambavyo vinawatia hasara wakulima na kubainisha watakao kamatwa, serikali itawachukulia hatua kali za kisheria.

Nao baadhi ya wakulima, akiwamo Boniface Mbasa, walisema wanafurahi kupewa mafunzo hayo ya matumizi sahihi ya viuatilifu na kukiri walikuwa wakikosea matumizi huku wakiiomba serikali idhibiti uingizwaji wa viuatilifu feki hapa nchini.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kongole walinda usalama kumtoa shabiki kiungwana

**WIKI** iliyopita tuliandika kuhusu tukio la ajabu lililotokea Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi kwenye mechi kati ya KMC FC na Simba, ambapo mlinda usalama uwanjani hapo alionekana akimpiga mateke shabiki mmoja aliyevuka eneo la kukaa mashabiki na kwenda kushangilia bao la nne pamoja na wachezaji wa timu hiyo.

Kwenye mechi hiyo ya Ligi Kuu iliyochezwa Desemba 24, mwaka jana ambayo Simba ilishinda mabao 4-1, shabiki huyo alikuwa na furaha iliyopitiliza iliyomfanya kuruka na kuingia eneo lisiloruhusiwa kwenda kwa wachezaji wa Simba waliokuwa wakishangilia, lakini furaha yake ikageuka kuwa majonzi baada ya kukutana na kipigo kikali cha mbwa mwizi, 'akikatwa mitama' na mmoja wa walinda usalama uwanjani hapo, kitu ambacho kilileta malalamiko makubwa kutoka kwa wadau wa soka nchini Tanzania na hata nje ya mipaka.

Kwa hakika tukiwa wadau wa michezo, tulilaani vikali kitendo hicho na tukilitaka Shirikisho la Soka nchini (TFF), kutoa elimu kwa watu wa usalama kutotoa vipigo kwa mashabiki wanaoshindwa kuzuia hisia zao na kuingia uwanjani, na badala yake kuwatoa kwa usalama kwa kuwa si maadui, lakini tulikemea vikali tabia hiyo ya mashabiki kuingia uwanjani.

Hata hivyo, juzi tena kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, katika mechi ya Simba dhidi ya Azam FC, lilitokea tena tukio kama hilo, baada ya shabiki mmoja kuvamia uwanjani, safari hii siyo kushangilia bao, yeye alikwenda kuonyesha 'mahaba' yake makubwa kwa kumkumbatia kipa namba moja wa timu ya Simba na Taifa la Tanzania, Taifa Stars, Aishi Manula.

Inawezekana kabisa kuwa wahusika walisoma maoni yetu, kwani wanausalama wa uwanja huo waliingia na kumchukua kijana huyo kistaarabu na uungwana wa hali ya juu na kisha kumtoa nje bila mvutano wala kipigo cha aina yoyote.

Nipashe tunatoa kongole kwa uungwana uliotumiwa na wanausalama wa uwanja huo kwa kitendo walichokifanya ambacho hakionyeshi tu kuwa ni cha kistaarabu, lakini kinaziambia hata nchi zingine za nje ya nchi kuwa Tanzania ni moja kati ya nchi ambazo zinathamini utu wa mtu.


Kumpiga mtu, mateke na kumswaga kama ng'ombe kama walivyofanya wanausalama wa Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora, kunadhalilisha utu wa mtu na kujenga hofu kwa wapenda soka kuhudhuria uwanjani hasa wale wenye mihemko mikubwa na timu zao.

Lakini kitendo kama kile kinamdhalilisha mtendwa mbele ya familia yake ambayo hata kama haikuwapo pale pengine ilikuwa ikishuhudia kupitia televisheni ama kwa kuhadithiwa baada ya tukio lile. Si kwamba tunaunga mkono vitendo vya mashabiki kuvamia uwanja, la hasha. Tunavikemea kwa nguvu zote na kuvipinga vikali huku tukitaka mashabiki wenye mihemko kujitahidi kujizuia, lakini pindi inapotokea tukio kama hilo, basi busara itumike kama ambavyo wamefanya wanausalama katika mechi kati ya Simba na Azam juzi Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Ni kwa sababu wataufanya mchezo wa soka si tu uonekane wa kiungwana, lakini kuwafanya mashabiki waliopo uwanjani wajione wako salama na amani zaidi, na kusababisha watu wengine zaidi kuupenda na kuzidi kumiminika viwanjani, hasa wanawake na watoto ambao wanaandaliwa kuwa mashabiki wakubwa wa kesho.

Tunaamini wanaoshindwa kujizuia na kuingia uwanjani kuonyesha hisia zao, si maadui na wengi wao hawana nia ovu ya kwenda kuwadhuru wachezaji, hivyo TFF izidi kutoa darasa kwa walinda usalama, ili kuzidi kuufanya mchezo wa soka kuwa burudani na rafiki kwa kila mmoja anayehudhuria uwanjani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kuelekea makundi CAF Simba itafute dawa ya ukosaji penalti

Na Adam Fungamwango

**KULIKUWA** na utani unaendelea kwenye mitandao ya kijamii kuwa kabla ya Rally Bwalya kupiga penalti, kuna baadhi ya mabeki wa Azam FC walikuwa wameingia kwenye boksi ambapo haitakiwi, hivyo ilibidi irudiwe.

Tukio hilo lilitokea jana wakati wa mechi ya Ligi Kuu kati ya Simba na Azam FC, Wekundu wa Msimbazi wakishinda mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Wakati wengine wakidai penalti ilistahili kurudiwa, kuna walisema kuwa hata ingerudiwa ingekoswa pia. Wapo walienda mbali zaidi kuwa hata ingerudiwa mara tano, mpigaji angekosa. Utani uliendelea baadhi wakasema hata wangebadilisha mpigaji, hali ingekuwa vile vile, wangekosa tu.

Simba imekuwa ikikosa penalti kwa namna ya kushangaza. Imekuwa ikitengeneza sana adhabu ya penalti kutokana na kuwa na wachezaji wasumbufu na wenye kasi, lakini zinapopatikana, kuzitumia ndiyo inakuwa tatizo.

Inavyoonekana kwa sasa ni kwamba timu hiyo haina mpigaji penalti maalum na wengi wao wanabahatisha. Bwalya, ambaye alipata penalti kwenye mechi dhidi ya Polisi Tanzania na kuipa timu yake ushindi wa bao 1-0, ndiye aliyekosa juzi.

John Bocco, ambaye kwa misimu yote aliyojiunga Simba ndiye tegemeo kubwa kwa upigaji mikwaju hiyo, siyo tu kwamba anaonekana kupoteza namba kwenye kikosi cha kwanza, lakini pia hata upigaji wake nao umeanza kuwa si wa uhakika.

Alikosa penalti kwenye mechi ya ufunguzi wa Ligi Kuu, Simba ikicheza dhidi ya Biashara United katika Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara na kuifanya timu yake kukosa ushindi kwa kutoka suluhu, lakini mpigaji mwingine maalum Erasto Nyoni ambaye ni nadra sana kukosa, naye alifanya hivyo kwenye mechi dhidi ya Ruvu Shooting, ingawa Simba ilishinda mabao 3-1.

Inavyoonekana ni kwamba wapiga penalti wa kutegemewa wa Simba, Bocco na Nyoni, wamepoteza namba lakini uwezo wa kupiga penalti pia. Kwanza kabisa tuelewe kuwa kupiga penalti ni kipaji. Kuna wachezaji hata kama wana uchezaji wa kawaida tu, lakini linapokuja suala la kupiga tuta ni mafundi.

Simba kwa miaka mingi nyuma ilikuwa ndiyo timu iliyokuwa na wachezaji wengi wenye uwezo wa kupiga penalti, kiasi cha timu nyingi kuhofia hata kwenda nayo hatua ya matuta, ikiwamo hata watani zao wa jadi, Yanga.

Nakumbuka Simba ilicheza mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika mwaka 1993, ambao ilifika fainali, moja ya timu iliyoitoa ni Santos ya Afrika Kusini, ambapo ilishindwa kwa mikwaju 11-10 ya penalti.

Ni mechi ambayo wachezaji wote wa Simba hadi kipa walitumbukiza mpira ndani ya wavuni, huku Santos wakikosa moja, Wekundu wakisonga mbele.

Kwa sasa sijui kama inaweza kuwa hivyo. Simba ipo kwenye hatua ya makundi Kombe la Shirikisho Afrika, hivyo benchi la ufundi wanaweza kukaa na wachezaji wao kuangalia ni jinsi gani wanaweza kufanya ili kutokosa ovyo penalti.

Ikumbukwe hata kwenye mechi ya mtoano ya Kombe la Shirikisho, Simba ilikosa penalti, Bernard Morrison akipiga penalti dhaifu iliyookolewa na kipa kama ilivyopigwa kwa Bwalya juzi.

Kocha Mkuu Pablo Franco, sasa akae na kuangalia mazoezini ni mchezaji gani ambaye anaweza kumpa jukumu la kupiga adhabu hiyo, kwani Simba inaweza kufika mbali, robo fainali au nusu fainali, halafu inapata penalti dakika za mwisho, upigaji wenyewe ndiyo ule, hivyo kuwasababishia majonzi na simanzi mashabiki wake.

Timu hiyo ina wachezaji wazuri wa kupiga penalti ambao ninawafahamu, lakini kwa bahati mbaya mara nyingi hawaanzi, pia huwa hawapewi jukumu la kupiga kwa sababu si maarufu.

Wachezaji hao ni Israel Mwenda, Gadiel Michael, na Hassan Dilunga. Ni wapigaji wazuri sana wa mikwaju ya penalti, lakini kwa sababu hizo ndiyo maana hawapigi.

Selemani Matola ambaye ni kocha msaidizi, anaifahamu Simba ile ya zamani ambayo ilikuwa na mafundi wa kupiga penalti wakati anacheza mpaka sasa, aongee na kocha Pablo waanze kulifanyia kazi suala hilo, kwani halionekana kubwa sana kwa sababu mechi nyingi ilizokosa timu ilikuwa inashinda, lakini siku ikitokea hasa kwenye mechi za kimataifa timu ikapoteza, ndipo kushtuka wataona kuwa kuna tatizo hilo.



Wanafunzi wa darasa la uhandisi kwenye kempu ya Boot inayoendelea katika Kituo cha Sayansi Kisosora wakijifunza jinsi ya kuchukua data kwa 'drone' na kuziingiza kwenye mfumo wa GIS. Wanafunzi hao wametengeneza 'appu' ya simu ambayo inaonyesha vituo vya afya vya Jiji la Tanga, na huduma zitolewazo maeneo husika. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Ujenzi wa SGR watumia trilioni 14.7

**Na Happy Severine,** BARIADI

MKURUGENZI wa Shirika la Reli nchini, Masanja Kadogosa, amesema ujenzi wa reli ya kisasa umetumia zaidi ya Sh. trilioni 14.7.

Kadogosa alisema hayo jana wakati wa ibada maalum ya kuliombea Taifa na Rais, Samia Suluhu Hassan iliyofanyika katika kijiji cha Mwakibuga, wilayani Bariadi, mkoani Simiyu.

Alisema kuwa reli hiyo ya kisasa itadumu miaka mingi na kutumika na vizazi vya sasa na vijavyo.

"Tanzania ni moja ya nchi chache zinazojenga reli ya kisasa kati ya nchi nyingi duniani na ujenzi reli za kisasa ni gharama kubwa hivyo Watanzania tunabahati kubwa sana na reli hiyo itasaidia kukuza uchumi wa nchi," alisema Kadogosa.

Awali, akitoa mahubiri katika misa hiyo maalumu, Padri Izengo Albert, kutoka Kigango cha Old Maswa, alisema reli hiyo italeta maendeleo na kufungua uchumi wa taifa.

"Ni matumaini yetu kuwa reli ya kisasa itakapokamilika itafungua mipaka ya uchumi na Watanzania wote tutanufaika sana na reli hiyo ikiwa ni sambamba na kumwombea mkurugenzi wa reli hiyo ili aweze kukamilisha kazi aliyokabidhiwa," alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, alisema takribani karne nzima ujenzi kama huo haujawahi kufanyika na kwa sasa ni jambo la kujivunia na kuipongeza serikali kwa jitihada za kuwaletea wananchi maendeleo.

Aidha, aliwataka wananchi kuendelea na majukumu mengine ya kujiletea maendeleo, ili kuunga mkono jitihada zote zinazofanywa na Rais.

# Sababu watoto wenye ulemavu kichwa kikubwa yatajwa

**Na Sabato Kasika**

JAMII imekumbushwa kuzingatia umuhimu wa lishe bora, ili kukabiliana na tatizo la watoto kuzaliwa na ulemavu ukiwamo wa kichwa kikubwa na mgongo wazi.

Wito huo ulitolewa jijini Dar es Salaam jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi isiyo ya kiserikali ya Child Help Tanzania, Janet Manoni, wakati akitoa salamu za mwaka mpya 2022.

Alisema, ulemavu wa mgongo wazi unaweza kuzuilika iwapo jamii itazingatia ulaji bora wa mlo kamili hasa vyakula vyenye wingi wa vitamini ya folik ambavyo vimethibitishwa kuwa na uwezo wa kuzuia kwa takribani asilimia 72 matatizo yahusuyo mishipa ya fahamu.

"Wakati huu ambao tunaelekea katika Wiki ya Kampeni ya Vitamini ya Foliki, jamii ikizingatia matumizi sahihi, tunaweza kupunguza kwa kiwango kikubwa uzazi wa watoto wenye ulemavu wa mgongo wazi, na tumepunguza pia idadi ya watu wenye ulemavu nchini kwetu na duniani," alisema Manoni.

Alisema, upo uhusiano mkubwa baina ya lishe duni, umaskini na ulemavu, na jamii maskini inakabiliwa na lishe duni ambayo matokeo yake ni pamoja na uzazi wa watoto dhaifu, waliodumaa na wenye ulemavu kama kichwa kikubwa na mgongo wazi.

"Uzuri kwa Tanzania, tuna vyakula vingi vyenye wingi wa vitamini ya folik, changamoto kubwa ni uelewa duni wa masuala ya lishe, hivyo kupitia wiki ya Folik, tutaelimisha jamii kuhusu umuhimu ya vitamin ya folik na ulaji bora, ili kujenga jamii yenye afya na ustawi," alisema.

Mratibu wa mawasiliano wa asasi hiyo, Milton Byemerwa, alisema, kuna umuhimu wa wadau kuwekeza katika elimu kwa umma kuhusu lishe bora ili kuiokoa jamii na uzazi wa watoto wenye ulemavu utokanao na njaa iliyofichika hasa mgongo wazi.

Kwa mujibu wa Byemerwa, mkakati huo utazinduliwa leo jijini Dar es Salaam, ili kuungana na jamii ya kimataifa katika kuhamasisha matumizi ya Vitamini ya Foliki Acid ambayo imethibitishwa kitaalamu kuwa na uwezo mkubwa wa kupunguza kwa zaidi ya asilimia 72 ya uwezekano wa kuzaa mtoto mwenye ulemavu wa mgongo wazi (NTDs).

Alifafanua kuwa hatua hiyo siyo tu kuinua afya za kinamama, bali kuwa na uhakika wa uzazi wa watoto wenye afya bora, hali itakayoimarisha ustawi wa familia na kuipunguzia serikali mzigo mkubwa wa kuwekeza katika tiba kwa matatizo ambayo yanaweza kuyaepuka.

Mtaalamu wa lishe kutoka Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC), Walbert Mgeni, alisema, wajawazito wanatakiwa kuzingatia ulaji wa vyakula mchanganyiko vyenye madini ya chuma, vitamini ya foliki acid na vitamini B12 ambavyo baadhi yake ni asili ya nyama kama samaki, makini na dagaa.

"Vyakula vingine ni vile vinavyoboresha ufyonzaji wa madini ya chuma mwilini ambavyo baadhi yake ni vyenye vitamini C kuanzia matunda yenye uchachu ikiwamo ukwaju, machungwa na limau," alisema Mgeni.

Meneja wa Miradi ya Uongezaji virutubishi kwenye vyakula kutoka Shirikisho la Lishe Duniani (Global Alliance for Improved Nutrition (GAIN), Archard Ngemela, alisema upungufu wa damu kwa wajawazito ni tatizo linalochangia vifo nchini.

Alisema pamoja na kuwapo na sera na sheria mbalimbali za uongezaji virutubishi, bado jamii kubwa haijafikiwa na elimu hiyo.

# Taarifa za TMA zasaidia wakulima Kagera

**Na Faustine Feliciane**

KATIBU Tawala wa Mkoa wa Kagera, Prof. Faustine Kamuzora, amesema taarifa za hali ya hewa zimewasaidia wakulima kujipanga kwa kilimo na majanga mengine yatokanayo na athari za mvua.

Akizungumza na Nipashe, Prof. Kamuzora alisema msimu huu wa mvua walichukua tahadhari zote tangu mapema, ikiwa ni pamoja na kuwashauri wananchi wa mkoa huo kulima mazao yanayokomaa kwa muda mfupi.

"Kagera kama mkoa tumekuwa tukifuatilia kwa karibu sana taarifa za hali ya hewa zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), zimetusaidia kujilinda na kujipanga na athari zote za mvua, pale zinapokuwa nyingi au kuwa ndogo…msimu huu tulitaarifiwa kuwapo kwa uhaba wa mvua tulijipanga na tumepata na tunaendelea kupata matokeo chanya," alisema Prof. Kamuzora.

Aidha, alisema kwa msimu huu kwa mkoa huo hali ya mvua si mbaya na zimenyesha kwa wastani na wananchi wamepata mazao mengi kama viazi na mengineyo.

"Bado tunaendelea kupata mvua za wastani, lakini kama mkoa tunaendelea kufuatilia taarifa za TMA, hata sasa wanaposema mvua Kanda ya Ziwa zitaendelea Januari hii, bado tunaendelea kufuatilia taarifa zao kwa karibu," alisema.

Aidha, katika hatua nyingine alisema mkoa huo kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) wanatafuta teknolojia ya kuwasaidia wananchi wa Kagera njia ya kuhifadhi zao la ndizi.

Prof. Kamuzora alisema mkoa wake umekuwa ukizalisha ndizi kwa wingi na wakati mwingine mazao yanapokuwa mengi ujikuta yakiharibikia shambani hivyo wanatafuta namna ya kuhifadhi mazao hayo kuanzia shambani.

"TARI watatusaidia ni teknolojia gani ambayo itawasaidia wananchi wetu kuhifadhi ndizi kuepuka kuharibika pale yanapovunwa kwa wingi, kwa sasa katika kila wilaya ya mkoa wetu kuna wataalamu kutoka kwenye taasisi hiyo wakitusaidia," alisema Prof. Kamuzora.

Alisema waliongeza uzalishaji wa ndizi na kuwa mkoa wa kwanza wa kuzalisha ndizi nchini na wanatafuta namna ya kuongeza masoko nje ya mkoa huo na nje ya Tanzania.

HABARI KITAIFA

# Wazazi kutohudhuria kliniki kwasababisha vifo watoto 436

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WATOTO wachanga 436 katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, wamepoteza maisha kutokana na wazazi wao kutohudhuria kliniki kwa wakati na kutofuata kanuni za afya kipindi cha ujauzito wao.

Watoto hao wamefariki katika kipindi cha mwaka 2021 kuanzia mwezi Januari hadi Desemba huku vifo vya wajawazito vikiwa tisa, sababu ikitajwa kutumia dawa za kuongeza uchungu na kutibu ugonjwa wa minyoo kipindi cha ujauzito.

Kadhalika katika kipindi hicho watoto 31 wamezaliwa wakiwa na ulemavu wa vichwa vikubwa, mgongo wazi, tumbo wazi, matege na matatizo mengine kutokana na mama zao kuchelewa kuhudhuia kliniki kwa zaidi ya miezi mitatu na kushindwa kutumia dawa vyema wanazopatiwa kipindi cha ujauzito.

Mratibu wa Mama na Mtoto wa Halmashauri ya Manispaa hiyo, Caroline Maliseli, alisema hayo wakati akizungumza na gazeti hili wanavyoshirikiana na wadau wa afya na waganga wa tiba asili kumaliza tatizo hilo.

Alisema, wajawazito waliojifungua mwaka jana katika hospitali ya halmashauri hiyo walikuwa 16,008, watoto waliozaliwa wakiwa na mwili ulioharibika na kufariki 115, waliokwisha kufariki 111, waliozaliwa na kufa ndani ya siku saba 58 huku vifo vya kinamama vitokanavyo na uzazi vikiwa tisa.

Maliseli alisema, vifo vya watoto chini ya mwezi mmoja vilikuwa sita, chini ya mwaka mmoja 29 na chini ya miaka mitano vikiwa 105, huku mwaka juzi vifo vya watoto na kinamama vikiwa 456 sawa na ongezeko la vifo 10 kwa mwaka huu.

Alisema, moja ya sababu kuwapo kwa wingi wa vifo hivyo ni kutokana na wajawazito kutokudhuria kliniki kwa wakati na wakati mwingine kutumia dawa za miti shamba kuongeza uchungu au kutibu ugonjwa wa minyoo hali inayosababisha mfuko wa uzazi kupasuka na mtoto kunywa maji machafu.

"Hivi karibu aliletwa mjamzito akiwa katika hali mbaya akiwa ametumia dawa za mitishamba kuongeza uchunguzi, tulimsaidia na tukamwokoa yeye, lakini mtoto tayari alikuwa ameshapoteza maisha akiwa tumboni na dawa hizi wanapewa na wazazi wao majumbani," alisema Maliseli.

Alisema, ili kuondokana na tatizo hilo mjamzito anatakiwa kuhudhuria kliniki baada ya kupata dalili za ujauzito wake na kuhakikisha anahudhuria vipindi vinane kwa kipindi chote cha ujauzito na muda utakapofika wa kujifungua ahakikishe anajifungulia katika kituo cha afya kilichoko jirani yake na sio majumbani au kwa waganga wa jadi.

Alisema kipindi cha mwezi Januari hadi Desemba mwaka jana, watoto 31 walizaliwa wakiwa na ulemavu wa vichwa vikubwa, mgongo wazi, tumbo wazi na matatizo mengine.

Aidha, Maliseli, aliwataka wenyeviti wa serikali za mitaa kwa kushirikiana na watendaji wa kata kujiwekea sheria ya kuwabana wajawazito wasiohudhuria kliniki kipindi cha ujauzito ikiwa ni pamoja na wale wanaokimbilia kwa waganga wa jadi kujifungua badala ya kufika katika vituo vya afya kupunguza wimbi la vifo kwa wajawazito na watoto.




Mkuu wa Chuo cha Ardhi Morogoro (ARIMO), Huruma Lugalla (wapili kulia), akikagua sehemu ya vigingi vitakavyotumika kwenye urasimishaji makazi holela katika Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya mwishoni mwa wiki. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# 'Wazazi epukeni kulaza watoto na watu wazima'

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JESHI la Polisi Mkoa wa Njombe, limetoa tahadhari kwa jamii kutoruhusu watoto wao kulala na watu wazima ili kuepuka kufanyiwa vitendo vya ukatili hasa wa kingono.

Tahadhari hiyo ilitolewa na Kamanda wa Polisi mkoa huo, Hamisi Issah, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu masuala mbalimbali yakiwamo pia yanayohusu watoto kulindwa.

"Tunasema kila siku kwamba watoto wadogo wanahitajika kulindwa na mnapokuwa mnawalaza usiku wasilale na watu wengine wakubwa ingawa ni wanafamilia, walale peke yao na watu wakubwa walale peke yao vinginevyo utakuta mtoto mdogo amefanyiwa ukatili," alitahadharisha Kamanda Issah.

Kwa mujibu wa Kamanda Issah, watoto wanapaswa kukaguliwa kila siku kuhakikisha wapo salama.

Alitoa rai kwa wazazi na walezi kutoruhusu watoto wao kutoka bila sababu ya msingi badala yake watulie nyumbani.

"Kwa kipindi hiki cha likizo wale wanaoruhusu watoto kwenda sehemu mbalimbali kutembea tafadhali achana na mtindo huo," alisisitiza Kamanda Issah.

Pia aliwakumbusha madereva wa magari na bodaboda kujua wajibu wao wawapo barabarani kwa kuangalia vivuko vya watoto na usalama wa watu wengine wanaoitumia barabara na kuepuka kufanya vitu kwa kuwakomoa watu au kwa kuwasababishia madhara mengine," alisema.

## Upepo waezua nyumba, zaidi ya 100 wakosa makazi

**Na Waandishi Wetu**

JUMLA nyumba 41 zimeezuliwa paa na upepo ulioambatana na mvua, mikoa ya Morogoro na Tanga na kusababisha zaidi ya watu 100 kukosa makazi.

Upepo huo pia umeathiri madarasa matatu ya Shule ya Msingi Kalengakelu, Tarafa ya Mlimba, wilayani Kilombero mkoani Morogoro.

Kaimu Ofisa Tarafa ya Mlimba, Acley Mhenga, alithibitisha athari hizo kutokana na mvua iliyonyesha mwishoni mwa Desemba 31, mwaka 2021.

Alisema pia, watu wawili wamejeruhiwa baada ya kuangukiwa na nyumba na kuiagiza kamati ya maafa ya eneo hilo kuangalia namna ya kuwasaidia wananchi.

Diwani wa Kata ya Kalengakelu, Martha Mkula, aliishukuru serikali kuwakimbilia baada ya maafa na kuomba hatua zaidi za haraka zichukuliwe ili kunusuru wananchi hao na kukarabati vyumba vya madarasa vilivyopata madhara ili shule zikifunguliwa wanafunzi wapate madarasa ya kusomea.

Katika tukio lingine watu 100 katika Kijiji cha Kwamatuku, wilayani Handeni mkoani Tanga, hawana makazi kutokana na mvua iliyoambatana na upepo, kubomoa zaidi ya nyumba na kuharibu miundombinu mingine.

Aidha, msichana Zakia Salimu anadaiwa kufariki baada ya kuzama kwenye mto wakati akitoka shambani.

Baba mzazi wa mtoto huyo, Salimu Mayoga, alisema mtoto wake alifariki dunia akitoka shamba wakati mvua hiyo ikinyesha.

Kwa upande wake, Katibu Tawala wilayani Handeni, Mashaka Mgeta, aliwatembelea wananchi hao na kuwapa pole na kuwataka kuwa watulivu wakati serikali inafanya jitihada za kuwasaidia.

■ **Imeandikwa na Idda Mushi, MLIMBA na Steven William, HANDENI**

# Waziri Ndumbaro aongoza mamia kusherehekea 2022 utalii wa ndani

**Na Amon Mtega,** SONGEA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, amewataka wakazi wa Mkoa wa Ruvuma kutumia vyema vivutio vya utalii vilivyoko kwenye mkoa kwa kufanya utalii ili waweze kutambua raslimali zilizoko.

Wito huo aliutoa jana wakati alipoongoza mamia ya wakazi wa Jimbo la Songea Mjini kwenda kusherehekea Mwaka Mpya wa 2022 kwa kufanya utalii wa ndani katika Hifadhi ya Misitu ya Milima Matogoro iliyopo Kata ya Ndilimalitembo, Manispaa ya Songea ambayo inahudumiwa na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS).

Dk. Ndumbaro, ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Songea, alisema wananchi wakijenga tabia ya kutembelea hifadhi zilizoko kwenye maeneo yao watapata elimu tosha ya kuzitambua raslimali zilizoko pamoja na kujenga ushirikiano wa kuzitunza.

Katika hatua hiyo nyingine Dk. Ndumbaro alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ikiwamo kutoa fedha kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii za kukarabati miundombinu ya maeneo ya vivutio ili kuimarisha utalii.

Katika suala la miundombinu kwenye maeneo ya Hifadhi ya Milima Matogoro, alisema wizara hiyo imejipanga kupitia fedha zilizotolewa na Rais Samia kujenga barabara ya uhakika itakayofika hadi juu ya misitu ya milima Matogoro ili kuwarahisishia wanaoenda kufanya utalii.

Akiwa katika milima ya Matogoro, aliwaonyesha wakazi wa jimbo maana halisi ya utalii kwa kuwagawia matunda ya porini yanayopatikana kwenye msitu huo yajulikanayo kwa jina la masuku ambayo hupendwa kuliwa na wanyama wa aina mbalimbali hasa nyani na binadamu.

Naye Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani Ruvuma, Oddo Mwisho, aliipongeza Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kujipanga kikamilifu kuleta mabadiliko makubwa kwenye suala la utalii ndani ya nchi.

Mwenyekiti huyo aliwapongeza Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kwa kufanya kazi ya kuhudumia Hifadhi ya Milima Matogoro ambayo pia ni sehemu ya vyanzo vya maji ambayo yanayotumika katika Manispaa ya Songea na pia ndiyo chanzo cha mto mkubwa uitwao Ruvuma ambao ndiyo uliobeba jina la Mkoa wa Ruvuma.

Kwa upande wake, Kamanda wa TFS Kanda ya Kusini, Manyisye Mpokigwa, alishukuru ushirikiano unaofanywa na ofisi ya Waziri wa Maliasili na Utalii katika kuendelea kuimarisha vivutio pamoja na kuzilinda hifadhi ikiwamo ya misitu.

Naye Diwani wa Kata ya Majengo Manispaa ya Songea, Abdulqadir Hussen, alisema kilichofanywa na Mbunge wa Jimbo hilo ni elimu tosha kwa wakazi wa Jimbo la Songea kwa kuwa wengi hawakujua kama milima ya Matogoro ni kivutio kizuri ikiwamo hali ya hewa iliyopo.

Katika utalii huo wamepata fursa ya kupata kitoweo cha nyama ya pori (nyati) bure kwa lengo la kutoa elimu kwa wakazi hao umuhimu wa kulinda raslimali zilizoko ili vitoweo viendelee kupatikana hadi kwa vizazi vijavyo.




Mkuu wa Wilaya ya Moshi Mjini mkoani Kilimanjaro, Abbas Kayanda (watatu kushoto), akikabidhi ufunguo wa gari aina ya Suzuki S Presso kwa Shemmy Chisumo, baada ya kuibuka mshindi wa kwanza wa promosheni ya Vodacom Tusua Mapene, kwenye viwanja vya Manyema, Mbuyuni wilayani humo juzi. Sambamba na zawadi hiyo, washindi 6 walijishindia Tv za kisasa na 10 simu janja kutoka promosheni ya "Show Love, Tule Shangwe". Kulia ni Mkuu wa Vodacom Kanda ya Kaskazini, George Venanty. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uuaji tembo kuonyesha ushujaa wadhibitiwa

**Na Ashton Balaigwa, MANYARA**

IMANI ya kabila la Waberbaig mkoani Manyara ya kila mwisho wa mwaka kuua tembo kama ishara ya ushujaa na kisha kujichagulia wanawake wanaotaka, imechangia vitendo vya ujangili katika Hifadhi ya Taifa ya Tarangire.

Mhifadhi wa hifadhi hiyo, Willium Maregesi, alisema hayo wakati akitoa taarifa ya hatua ya kuvidhibiti vitendo vya ujangili kwa Waandishi wa Habari wa Mazingira (JET), waliotembelea hifadhi hiyo ikiwa ni sehemu ya mafunzo kwa vitendo.

Mafunzo hayo yametolewa na Mtandao wa Ufuatiliaji wa Biashara Viumbepori Halali na Haramu katika nchi za Afrika Mashariki (TRAFFIC), kwa ufadhili wa hisani ya watu wa Marekani (USAID) chini ya mradi unaofahamika kama CONNECT.

Mhifadhi Maregesi, alisema katika kipindi cha miaka mitano watu wa kabila la Waberbaig walikuwa wakiingia katika hifadhi hiyo na kuhakikisha wanaua tembo na kukata mkia na kurudi nao kijijini na kufanyiwa sherehe kubwa.

"Kulikuwa na ujangili huo unaotokana na imani za kabila la Waberbaig, mtu anaingia hifadhini na kuua tembo na kukata mkia na kurudi kijijini kwake akifika huko anaonekana ni shujaa na anafanyiwa sherehe na kuchagua mwanamke yeyote hapo anayemtaka na kumuoa," alisema.

Hata hivyo, alisema katika miaka ya hivi karibuni vitendo hivyo vya ujangili wa tembo vimedhibitiwa kwa kiwango kikubwa na watuhumiwa wakifikishwa mahakamani na kuhukumiwa.

Kwa upande wake, Ofisa Programu kutoka TRAFFIC, Allan Mgaza, alisema kuna umuhimu wa kuendelea kutoa elimu ya uhifadhi kwa wananchi wanaoizunguka ili kuona kama wao ni sehemu yao na kuendelea kutunza maliasili hali itakayowafanya kuachana na vitendo vya ujangili kwa viumbehai hao.

Alipongeza juhudi za hifadhi hiyo ya Tarangire ya kudhibiti vitendo vya ujangili wa tembo katika miaka ya hivi karibuni na kuwataka kuongeza nguvu zaidi kwa wanyama wengine ili kuendelea kulinda maliasili kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

Ofisa Mhifadhi Mwandamizi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori -Tanzania (TAWA), Wilbright Munuo, alisema licha ya kuwapo kwa ujangili wa wanyama, kuna uvamizi mkubwa katika maeneo ya hifadhi hasa katika maeneo ya mapito ya wanyama na kwamba kuna muhimu kuwapo kwa sheria za kulinda maeneo hayo.

# Bil. 3/- zapitishwa kutengeneza miundombinu ya barabara Tarime

**Na Samson Chacha,** TARIME

BARAZA la Madiwani Halmashauri ya Mji Tarime, mkoani Mara limepitisha rasimu ya bajeti ya matengenezo ya miundombinu ya barabara kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ya Sh. 2,745,450,000.

Bajeti hiyo imepangwa kutengeneza barabara zenye jumla ya urefu wa kilomita 356,508, kati ya hizo 290,436 ni barabara za mlisho.

Kikao hicho cha kufunga mwaka kilifanyika Desemba 28, chini ya Mwenyekiti wake, Daniel Komote, Mbunge wa Viti Maalumu, Ghati Zephania, Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Gimbana Ntovya na kuhudhuriwa na kamati ya ulinzi na usalama.

Mhandisi wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA), Wilaya ya Tarime, Charles Marwa, alisema wakala huo umepanga kutumia Sh. 2,745,450,000 kwa matengenezo ya barabara na halmashauri ambayo ina jumla ya kilomita 356,506.

Alisema kuwa bajeti ya ukarabati wa barabara na usimamizi itatumia Sh. 720,450,000 kutoka mfuko wa barabara wa Sh. 1,000,000,000 fedha za maendeleo nyongeza ya bajeti kwa kila jimbo Sh. 500,000,000, fedha za maendeleo kutokana na tozo ya mafuta Sh. 500,000,000 na fedha za usanifu na ufuatiliaji miradi ya maendeleo Sh. 25,000,000.

Alisema katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 TARURA Halmashauri ya Mji Tarime, ilitengewa Shilingi bilioni mbili na mwezi Desemba 2021 imepokea Sh. 98,897,897.71, na Sh. 116,500,000 ni tozo ya mafuta za maendeleo.

Alisema changamoto zinazoikabili TARURA ni pamoja na wananchi kupitisha mifugo yao, mvua zinazoendelea kunyesha mara kwa mara wilayani Tarime na kuharibu miundombinu, magari makubwa zaidi ya tani 10 kuchangia kuharibu barabara.

Katika kikao hicho madiwani hao walieleza kutoridhishwa na ujenzi chini ya kiwango wa barabara mbili zilizojengwa mjini kwa kiwango cha lami kilomita moja karibu na uwanja wa mpira na barabara ya Kanisa Katoliki kwa gharama ya Sh. 650,000,000 na mkandarasi ameshapokea malipo ya kwanza ya Sh. 232,807 885.00.

# Wafurahia serikali kufunga machinjio ya punda

**Na Friday Simbaya**, IRINGA

BAADHI ya wananchi na wadau wa sekta ya mifugo wilayani Iringa, wameipongeza serikali kwa kufunga biashara ya punda pamoja na machinjio yake ambayo ilikuwa inafanywa na wawekezaji kutoka nchini China waliotegemea wanyama hao kutoka katika maeneo mbalimbali ya nchi na kusababisha kuongezeka kwa wizi wa wanyamakazi hao.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, walisema kuwapo kwa viwanda vya kuchinja punda kulisababisha kuongezeka kwa wizi wa punda katika maeneo mbalimbali nchini na kuhatarisha usalama wa wanyama hao.

Walisema uwapo wa viwanda hivyo vya kuchakata ngozi ya punda nchini unaaminika kuchangia wizi wa punda na kuzitia shakani familia zinazowategemea wanyama hao kwa shughuli za usafirishaji, kilimo, za nyumbani na pato la kila siku.

Rodha Mwangosi, mkazi wa Kijiji cha Migoli, wilayani Iringa ameipongeza serikali kwa kufunga machinjio zote za punda nchini kwa kuwa zilichochea wizi wa punda katika kijiji chao. Aliongeza kuwa amekuwa mmoja wa waathirika wa biashara hiyo, kwa kuwa aliibiwa punda wawili kati ya wanne aliokuwa anamiliki awali. Redenta Mgungile, mkazi wa Kijiji cha Mtera, alisema serikali imesikia kilio chao na baada ya kusitisha biashara hiyo ya punda sasa watazaliana kwa wingi kwa kuwa hawataibiwa tena.

Mgungile aliongeza kuwa kuwapo kwa viwanda hivyo, kuliongeza mzigo wa kuwalinda punda kwa vile walikuwa wanalazimika kuwalipa wafanyakazi kati ya Sh. 30,000 hadi Sh. 40,000 kwa kuhofia wezi huo.

Naye Mratibu wa Mradi wa Ustawi wa mnyamakazi punda toka Inades Formation Tanzania, Fortunata Tarimo, alisema punda ana mchango mkubwa kwa ustawi wa familia za wafugaji na wakulima wadogo kwa kuwa wanatumika kwa shughuli mbalimbali za kijamii na kinamama ndiyo wanufaika wakubwa.

Pia alisema kuwa kuwapo kwa punda katika jamii kutasaidia kampeni ya kumtua mama ndoo kichwani kwa kuwa wanawake ambao mara nyingi hufanya kazi ya kuchota maji wanayapata kutoka katika umbali mrefu.

Alisema kumekuwapo na malalamiko kutoka jamii mbalimbali ya uwapo wa viwanda vya kuchakata mazao ya punda na ukiukwaji wa masharti ya mkataba pamoja na kanuni za ustawi wa wanyama.

"Kuibiwa punda ni kupoteza rasilimali kubwa ambayo kwa sasa a ni ngumu kupatikana kiurahisi kwa mtu mwenye kipato kidogo baada ya gharama za punda kuongezeka na kufikia wastani wa Sh. 250,000 kwa punda mmoja," alisema.



Ofisa Huduma kwa Wateja wa Benki ya NMB, Neema Kazoviyo, akizungumza na mmoja kati ya washindi 22 waliojishindia pikipiki ya magurudumu matatu katika droo ya fainali ya 'Bonge la Mpango 2merudi Tena' iliyochezeshwa Bagamoyo mkoani, Pwani. Katikati ni Meneja wa Benki ya NMB Bagamoyo, Bertha Mungure na Ofisa Mkaguzi Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, Pendo Mfuru. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Halmashauri Kahama yatoa mkopo mil. 64/-

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

HALMASHAURI ya Manispaa ya Kahama, mkoani Shinyanga, imetoa mikopo isiyokuwa na riba kwenye vikundi 20 vya watu wenye ulemavu, wenye thamani ya Sh. milioni 64.2 ili kuvikwamua kiuchumi na kuondokana na changamoto ya ukosefu wa mitaji na ombaomba mitaani.

Fedha hizo zimetolewa kwa kipindi cha mwaka wa fedha kuanzia 2018/2019 hadi mwaka 2020/2021 na zinatokana na mapato ya ndani ya halmashauri hiyo ya asilimia 10.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa halmashauri hiyo, Robert Kwela, aliyabainisha hayo juzi wakati akizungumza na gazeti hili ofisini kwake namna wanavyotoa mikopo kwa wajasiriamali hasa wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na kuwasimamia na kuhakikisha wanakuwa kimitaji.

Alisema, halmashauri imetoa mikopo ya Sh. milioni 64.215 kwenye vikundi 20 vya watu wenye ulemavu huku mwaka wa fedha 2018/2019 ikifanikiwa kutoa Sh. milioni 15 kwa vikundi saba na mpaka sasa vimesharejesha Sh. milioni 11.588.

Pia alisema mwaka wa fedha 2019/2020 walitoa mikopo katika vikundi viwili vya wajasiriamali wenye ulemavu Shilingi milioni tano, vimerejesha Sh. milioni 3.33 bado vinadaiwa Sh. milioni 2.97 na hakuna kikundi ambacho hakirejeshi.

Vile vile, alisema mwaka wa fedha 2020/2021 walivipatia vikundi vinane vya mkopo wa kiasi cha Sh. milioni 44.215 vimerejesha Sh. milioni 13.470, bado vinadaiwa Sh. milioni 30.745 na mwaka huu wa fedha 2021/2022 hawajaanza kutoa mikopo baada ya kuwapo kwa changamoto ya mifumo.

"Tumekuwa tukitenga fedha kupitia mapato yetu ya ndani kila mwaka kwa ajili ya wajasiriamali wetu, tumetoa mikopo ya Sh. milioni 64.215 kwa vikundi 20 vya watu wenye ulemavu kuanzia mwaka 2018/2019 hadi 2020/2021, vimerejesha milioni 24.361 na vimebakiza Sh.milioni 36.854," alisema Kwela.

Kwa upande wake, Katibu wa Shirikisho la Watu wenye Ulemavu Kahama (Shivywata), Zawadi Masoud alisema, mikopo inayotolewa na halmashauri imekuwa ikiwasaidia kuwakwamua kiuchumi kwa kuongeza mitaji kwenye biashara zao na sasa wanasaidiana tofauti na awali.

Alisema, mwaka jana wenye ulemavu wakutokusikia (viziwi), walipata mkopo wa Sh. milioni 25 ambazo waliziwekeza kwenye biashara zao na sasa wanaendelea na marejesho ili kuwapatia fursa wengine kukopa fedha hizo na kuitaka halmashauri kuwashirikisha zaidi wakati wanapotoa mikopo hiyo ili wanaochukua wasijirudie.

Mmoja wa wanufaika wa mikopo hiyo, Edward John alisema, kabla ya kupatiwa mkopo huo hakuwa na shughuli ya kufanya, baada ya kupatiwa sasa ana biashara inayoendesha maisha yake.

# Hofu yatanda kuibuka wizi wa ng'ombe maksai

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wa Kijiji cha Kageme, Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, wameiomba serikali kuingilia kati kudhibiti wizi wa mifugo wakati wa usiku.

Wizi huo ni wa ng'ombe aina ya maksai wanaotumiwa kwa ajili ya kilimo cha kibiashara ikiwamo pamba na tumbaku.

Hayo waliyabainisha mwishoni mwa mwaka 2021 kwenye mkutano wa hadhara wa Mbunge wa Jimbo la Ushetu, Emmanuel Cherehani, aliyekuwa amembatana na wakuu wa idara wa halmashauri hiyo uliokuwa na lengo la kusikiliza na kutatua kero mbalimbali za wananchi katika kijiji cha Kangeme, Kata ya Ulowa.

Mmoja wa wakazi wa kijiji cha Kangeme, Lameck Lyanga, alisema kuibuka kwa wimbi la wizi wa ng'ombe hususan wanaotumika katika kilimo (maksai) nyakati za usiku kumezua hofu kwa usalama wa wafugaji na mali zao.

"Ng'ombe 10 wamepotea katika mazingira ya kutatanisha na mpaka sasa hakuna hatua zozote zilizochukuliwa, tunaomba serikali itusaidie kutokomeza wimbi hili ambalo linaturudisha nyuma kwenye shughuli zetu za kilimo," alisema Lyanga.

Naye Mariamu Masunga, alisema ijumaa iliyopita ng'ombe wake wawili waliibiwa na amejaribu kufuatilia kwa viongozi wa serikali za mtaa, lakini hajapata msaada wowote mpaka hivi sasa na kuiomba serikali kuingilia kati kumsaidia ili apate haki yake.

Alisema yeye ni mjane na alikuwa akiwatumia ng'ombe hao kwenye shughuli zake za kilimo, na kwamba ana hofu kwa msimu huu wa kilimo uzalishaji wake utashuka kutokana na kukosa nguvu kazi aliyokuwa anaitumia.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kijiji cha Kangeme, Sidini Mlangali, alikiri kuwapo kwa wizi wa mifugo na kudai uwapo wa mnada katika kata hiyo unachangia wizi wa mifugo na ameanzisha kikundi cha ulinzi wa jadi (sungusungu), lakini mwitikio wa wananchi kujitokeza kushiriki katika shughuli za ulinzi ni mdogo.

Vile vile, alisema suala la wizi limekuwa likijitokeza mara kwa mara na wamekuwa wakifuatilia, lakini ni vigumu kuwabaini wahalifu na kuwaomba wananchi kuendelea kutoa taarifa za siri kwa vyombo vya ulinzi na usalama ili kuwachukulia hatua kali za kisheria wale watakaobainika.

Mbunge Chereheni, aliwataka viongozi wa vijiji kuhuisha vikundi vya ulinzi shirikishi ili kudhibiti na kutokomeza matukio ya wizi wa mifugo ambao umeshamiri katika kijiji hicho unaotajwa kurudisha nyuma maendeleo ya wafugaji.

Cherehani alisisitiza, suala la ulinzi ni la kila raia na kila mwananchi anatakiwa kutoa taarifa za wahalifu katika vyombo vya ulinzi na usalama.

Alisema wezi wa ng'ombe hawatoki nje ya kata ya Ulowa, wengine ni watoto wa wafugaji na kutaka wasiwafiche kwa kuwa vitendo hivyo havivumiliki katika jamii.

Kadhalika alisema, atawasiliana na Mkuu wa Polisi Wilaya ya kipolisi Ushetu, ili kukamilisha ujenzi wa kituo cha polisi kata hiyo kuimarisha usalama.

Nipashe
Spotika



VIUNGO WA KATI 10 BORA MWAKA 2021 UK. 12 - 13



FATI NA GAVI

# NYOTA WATANO WAKUIREJESHA BARCA KATIKA UBORA WAKE

**BARCELONA,** Hispania

KUSHUKA kwa Barcelona katika miaka michache iliyopita kumeonekana sana. Ingawa msimu huu wamefikia kwenye hatua mbaya zaidi. Hakuna aliyeweza kuziba pengo ipasavyo baada ya kuondoka kwa Lionel Messi. Matokeo yake, 'Blaugrana' hao wamefichuliwa vibaya, na kwa sasa wanapitia moja ya misimu mibaya zaidi kuwahi kutokea.

Kwa mara ya kwanza baada ya miaka 17, Barcelona wameshuka kwenye Ligi ya Europa kutokana na kushika nafasi ya tatu katika kundi lao la Ligi ya Mabingwa Ulaya. Xavi Hernandez, ambaye amechukua nafasi ya Ronald Koeman kama kocha mpya, amekuwa akivuta kamba ili kuirejesha timu kwenye mstari. Hata hivyo, imeonekana kuwa kazi kubwa.

Hakujawa na mabadiliko yoyote makubwa katika suala la matokeo. Hata hivyo, kiungo huyo wa zamani wa Barcelona anaonekana kuiongoza timu katika mwelekeo sahihi. Kwa kweli, kwa kuzingatia yale ambayo tumeshuhudia katika wiki za hivi karibuni, inaweza kuwa suala la muda kabla ya Blaugrana kurudi walikokuwa.

Kwa kukosekana kwa wachezaji kama Messi, Luis Suarez na Antoine Griezmann, Barcelona itahitaji wengine kuweza kuwainua na kurudi kwenye ubora wao.

Hapa tunawaangalia wachezaji watano wanaoweza kuisaidia Barcelona, haya sasa...

### #5. FERRAN JUTGLA

Ferran Jugtla mwenye umri wa miaka 22, amekuwa akifanya vema kutokana na uchezaji wake katika mfumo wa vijana wa Barcelona. Alipata nafasi adimu kuiwakilisha Barcelona wakati wa mchezo wa ligi dhidi ya Elche wikendi iliyopita.

Licha ya kuanza kwa mara ya kwanza na timu ya wakubwa, raia huyo wa Hispania alionekana kuwa bora katika nafasi yake kuliko Memphis Depay na Luuk de Jong.

Jutgla hakupoteza muda katika kufanya mchango wake uonekane. Alifunga bao mapema kwenye mchezo huo, lakini iliamuliwa kuwa ameotea. Baadaye aliwafungia Blaugrana dakika ya 16, akiunganisha krosi ya Ousmane Dembele. Katika muda wake wote uwanjani, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, alikuwa tishio kubwa kwa safu ya ulinzi ya upinzani.

Mwendo wake, nafasi na silika yake ya kufunga mabao ndivyo Barcelona wanahitaji kwa sasa. Hakuna shaka anaweza kuleta mabadiliko kwa timu kwenda mbele.

### #4. ABDE EZZALZOULI

Abde Ezzalzouli alipandishwa katika timu ya wakubwa ya Barcelona na Xavi mwezi uliopita. Inashangaza kuona namna alivyoonyesha kiwango cha kuvutia katika wiki chache zilizopita. Abde amefunga mara moja na kusaidia moja katika mechi saba za klabu hiyo kufikia sasa.

Kinachomfanya winga huyo kujitokeza ni uwezo wake wa kuupeleka mchezo kwenye safu ya ulinzi ya wapinzani bila woga. Anawachana ili kuunda kitu kwa timu yake. Uchezaji wake wa kucheza chenga, kasi na kiungo ni wa kuvutia, na anaonekana kuwa na mustakabali mkubwa mbele yake.

### #3. DANI ALVES

Dani Alves alirejea Barcelona msimu huu wa majira ya joto kusaidia kujenga kizazi kijacho. Inaonekana amekuja kwa wakati ufaao. Kwa uzoefu wake, moyo wa kufanya kazi kwa bidii na mawazo ya kushinda, beki huyo wa kulia anapaswa kuleta mengi kwa timu na kuchukua jukumu muhimu katika ufufuo wake.

Licha ya kuwa na umri wa miaka 38, Mbrazil huyo bado hajaonyesha dalili za kupunguza kasi yake. Alikuwa mmoja wa wachezaji waliofanya vema zaidi alipoiwakilisha Barcelona katika pambano la kirafiki la hivi karibuni dhidi ya Newell's Old Boys. Uelewa wake wa kanuni za msingi za klabu ulionyeshwa muda wote wa mchezo, kwani alichangia kwa kiasi kikubwa katika kushambulia na kulinda.

Alves ataweza kushiriki katika michezo rasmi ya Blaugrana kuanzia mwezi huu, atakaposajiliwa na klabu hiyo. Kando na wakongwe wengine, Mbrazil huyo anatarajiwa kuwa na jukumu muhimu katika kukiongoza na kuzindua kizazi kijacho cha nyota pale Camp Nou.

### #2. GAVI

Gavi amekuwa mchezaji bora wa Barcelona tangu kampeni kuanza. Kiungo huyo alithibitisha jinsi alivyo na kipaji cha hali ya juu kutokana na uchezaji wake dhidi ya Elche. Alifunga bao la pekee la kuvutia, na kutoa dakika kadhaa za kuvutia.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 17, alitajwa kuwa mchezaji bora wa mechi kwa uchezaji wake mzuri kwenye mchezo huo. Ilikuwa ni siku nyingine nzuri tu ofisini kwa kijana huyo wa Hispania. Tayari ameichezea Barcelona mechi 21 hadi sasa msimu huu, na kuwavutia wengi.

### #1. ANSU FATI

Ansu Fati alipewa jezi namba 10 iliyoachwa wazi na Lionel Messi, jambo ambalo linaelezea kwa kiasi kikubwa jinsi Barcelona wana imani naye.

Mshambulizi huyo ameonekana kuwa mtu wa kutegemewa sana mbele ya lango, na yuko kwenye nafasi nzuri ya kuwa uso wa pili wa klabu hiyo.

## ISIKUPITE

KIPA wa Manchester United, David De Gea, ndiye mlinda mlango aliyeokoa mashuti mengi zaidi sasa msimu huu. Licha ya 'clean sheets' nne tu, De Gea ameokoa mashuti 57 kati ya 81yaliyoelekezwa langoni mwao, ameokoa mabao 7.6, akifuatiwa na kipa wa Wolverhampton, Jose Sa aliyekabiliana na mashuti 67 na kuokoa mabao 6.7 na Robert Sanchez wa Brighton & Hove Albion) alipambana na mashuti 64.



# VIUNGO WA KATI 10 BORA MWAKA 2021

**LONDON,** England

MARA kwa mara inasemwa kuwa timu zinazoshinda mapambano ya katikati ya uwanja kawaida hushinda mechi. Moja ya nafasi muhimu zaidi kwenye uwanja, viungo mara nyingi ndio wanaoutengeneza mchezo.

**Mwaka 2021 umeshuhudia wachezaji wa kati wa ajabu wakifanya maonyesho ya kupendeza kwenye uwanja. Kuanzia uchezaji mzuri wa N'Golo Kanté kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hadi Kevin De Bruyne akiwa na kiwango kizuri kwenye Ligi Kuu ya England, viungo wa kati wa mchezo huo wamefanya vema mwaka 2021.**

Makala haya inawaangalia viungo wa kati 10 bora zaidi kwa mwaka 2021, twenda sasa...

### #10. TONI KROOS (REAL MADRID)

Wachezaji watatu wa kiungo wa Real Madrid, Toni Kroos, Modric na Casemiro wanaweza kuwa wanazeeka, lakini hawaonyeshi dalili za kupunguza kasi. Mmoja wa wapiga pasi bora kuwahi kucheza mchezo huo, Kroos amekuwa na msimamo thabiti kwa Real Madrid mwaka huo.

Nyota huyo wa Real Madrid alionyesha kiwango cha kuvutia zaidi katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Liverpool mapema mwaka huo. Akiwa bado na umri wa miaka 31, Kroos ameanza msimu katika kiwango kizuri na amekuwa mmoja wa wachezaji bora wa Real Madrid. Kroos akiwa mtulivu na mwenye mpira, atakuwa na matumaini ya kuhamasisha Real Madrid kutwaa ubingwa wa LaLiga msimu huu. Pia atahitaji kuwa katika ubora wake wa kucheza wakati Real Madrid watakapomenyana na PSG katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora.

### #9. NICOLO BARELLA (INTER MILAN)

Mmoja wa viungo kamili katika soka la dunia kwa sasa, Nicolo Barella amekuwa na mwaka mzuri kule Inter Milan na Timu ya Taifa ya Italia. Akiwa amejaa mbio na ubunifu, Barella alifunga na kutengeneza mabao mengi muhimu katika mbio za Inter kutwaa taji la Serie A msimu uliopita.

Akiwa amewahi kuwapo katika kikosi cha Roberto Mancini cha Italia ambacho kilishinda Euro 2020, pia Barella amekomaa na kuwa mmoja wa wachezaji wa kutegemewa na wa kudumu kwa klabu yake na timu ya taifa.

Lakini, akiwa amebarikiwa uwezo mzuri wa kiufundi na maono ya ajabu, Barella ana uwezo wa kuchezesha wachezaji wenzake mipira. Ndiyo kwanza ana umri wa miaka 24, kiungo huyo wa kati wa Italia ana uwezo wa kufika mbali zaidi katika miaka ijayo.

### #8. MASON MOUNT (CHELSEA)

Mason Mount amejiimarisha kama mmoja wa viungo bora wa England wa kizazi hiki. Kiungo huyo mshambuliaji alicheza nafasi muhimu katika ushindi wa kihistoria wa Ligi ya Mabingwa Ulaya. Pia alivutia sana akiwa na England kwenye Euro 2020.

Akiwa na uwezo wa kukimbia, Mount huifanya timu ifurahie kwa kukimbia kwake kwa akili, pasi nzuri na uwezo wa kuona vizuri. Akiwa kipenzi cha mashabiki huko Stamford Bridge, tayari Mount ameanza msimu huu katika hali nzuri pia.

Katika mechi 16 pekee za Ligi Kuu England hadi sasa, kiungo huyo mkabaji mwenye umri wa miaka 22, amechangia mabao saba na kutoa asisti nne.

### #7. CASEMIRO (REAL MADRID)

Bila shaka ndiye kiungo bora zaidi wa ulinzi katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Casemiro amekuwa sehemu muhimu ya mwanzo mzuri wa Real Madrid kwenye LaLiga chini ya kocha, Carlo Ancelotti. Mtaalamu wa mchezo wa kuvunja, Casemiro pamoja na Luka Modric na Toni Kroos ameisaidia Real Madrid kutawala vita vya katikati ya uwanja dhidi ya wapinzani wengi.

Katika timu iliyojaa nyota, michango ya Casemiro mara nyingi hufunikwa. Hata hivyo, hakuna kukataa umuhimu wa Casemiro kwa Real Madrid na timu ya Taifa ya Brazil.

### #6. JORGINHO (CHELSEA)

Kiungo wa kati wa Chelsea, Jorginho amekuwa na mwaka wa kukumbuka. Mshindi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na Euro 2020, Jorginho alimaliza nafasi ya tatu kwenye tuzo ya Ballon d'Or 2021.

Mchezaji pasi mwenye kipaji cha kipekee, Muitaliano huyo anaweka hali ya mchezo na usambazaji wake na kuisaidia Chelsea na Italia kuamuru mchezo kutoka katikati ya uwanja. Penalti muhimu zilisaidia klabu yake na timu ya taifa kushinda mataji muhimu.

Akiwa na uwezo wa kuanzisha mashambulizi, Jorginho ni mmoja wa viungo muhimu wa timu hii mahiri ya Chelsea chini ya kocha, Thomas Tuchel. Itafurahisha kuona ikiwa Muitaliano huyo ataweza kuendeleza kiwango chake kizuri mwaka 2022.



DE BRUYNE

### #5. JOSHUA KIMMICH (BAYERN MUNICH)

Inaonekana kama uhalifu kumweka Joshua Kimmich kwenye namba pekee kwenye orodha hii. Tangu kuondoka kwa Thiago kuelekea Liverpool, Kimmich ameifanya nafasi ya 'namba 6' kuwa yake katika klabu ya Bayern Munich.

Kimmich kweli ni mchezaji wa kiwango cha dunia! Takwimu zake zinaeleza wazi kabisa.

Kuweka malengo na kuvunja mchezo kwa urahisi sawa, Kimmich amekuwa mmoja wa wachezaji bora wa Bayern Munich mwaka 2021. Kiungo huyo mahiri anaonekana kutulia vizuri katika nafasi ya kiungo mkabaji chini ya kocha Nagelsmann kule Bayern Munich.

Andrea Pirlo alikuwa mfalme wa kweli wa nafasi hii. Kama Kimmich ataendelea kucheza kwa njia ile ile, anaweza kuishia kuwa bora kama Muitaliano huyo.

### #4. N'GOLO KANTE (CHELSEA)

Kiungo wa kati wa Chelsea, N'Golo Kante ndiye mchezaji bora zaidi kwenye eneo hili.

Mfaransa huyu amekuwa na majeraha ya kusumbua mwaka huu na angeweza kuwa juu zaidi kwenye orodha kama angeendelea kuwa fiti.

Kiungo huyo wa kati wa Ufaransa pia ana uelewano mzuri na nyota wengine kama Jorginho na Mason Mount. Kocha Thomas Tuchel atatumaini nyota wake huyo kuwa fiti kwa hatua muhimu za msimu huu.

### #3. BRUNO FERNANDES (MANCHESTER UNITED)

Bruno Fernandes hajakuwa katika kiwango bora kabisa katika wiki chache zilizopita, hata hivyo, hakuna ubishi kwamba, mchango alioutoa Manchester United katika mwaka mzima wa Kalenda wa 2021 ni mkubwa.

Mfungaji wa mabao wa Manchester United kabla ya ujio wa Cristiano Ronaldo pale Old Trafford, Fernandes ana idadi ya kuvutia hata msimu huu. Kiungo huyo wa kati wa Ureno amefunga mabao matano na kutoa asisti tatu za mabao katika mechi 16 za Ligi Kuu England hadi sasa.

Fernandes ambaye anafahamika kwa ustadi wake kupitia mipira na mashuti ya mbali, atakuwa na matumaini ya kurejea katika ubora wake na kuisaidia Man United kupata nafasi ya nne bora kwenye Ligi Kuu England msimu huu.

### #2. THOMAS MULLER (BAYERN MUNICH)

Akicheza nafasi ya usaidizi kwa Robert Lewandowski kama kiungo mkabaji, Thomas Muller amekuwa bora kwa Bayern Munich mwaka wa 2021. Ingawa Lewandowski anaweza kupata sifa zote kwa mabao aliyofunga, Muller mara nyingi amekuwa karibu, kusaidia na kuwakokota mabeki.

Namba za Muller msimu huu kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, si za ajabu. Katika mechi 17, nyota huyo wa Ujerumani amefunga mabao matano, pia amefanikiwa kutoa asisti 13 za mabao.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 32, amekuwa na uhusiano mzuri na Lewandowski na Muller atakuwa na matumaini ya kuwa bora zaidi msimu huu.

### #1. KEVIN DE BRUYNE (MANCHESTER CITY)

Mmoja wa viungo bora zaidi kuwahi kucheza kwenye Ligi Kuu England, Kevin De Bruyne anachukua nafasi ya kwanza mbele ya Thomas Muller katika viwango vyetu.

Wakati kiungo huyo wa kati wa Ubelgiji akiuguza majeraha katika kipindi cha pili cha 2021, De Bruyne alikuwa katika kiwango kizuri kwenye Ligi ya England katika miezi michache ya kwanza hata kushinda tuzo ya Mchezaji Bora wa Mwaka wa PFA.

De Bruyne pia amerejea kwa nguvu kwenye Ligi Kuu mwezi huu, akifunga mabao mazuri dhidi ya Leeds United na Leicester City.

Manchester City watahitaji kiwango cha Kevin De Bruyne na kusukuma mashambulizi kutoka katikati ya uwanja ikiwa wanataka kupata taji la Ligi ya Mabingwa msimu huu.

## Nukuu

"Yuko katika viwango vya Cristiano Ronaldo sasa, winga wa mara moja ambaye amejipambanua kuwa mfungaji bora. Ikiwa mwaka 2021 ulikuwa wa kuvutia kwa Salah, 2022 unaweza kuwa hivyo zaidi. Anaonekana kuwa na uhakika katika hatua hii ya kushinda Mchezaji Bora wa Mwaka wa PFA, lakini kama Liverpool watashinda Ligi ya Mabingwa, atakuwa na nafasi nzuri ya kunyanyua Ballon d'Or," **Beki wa zamani wa Manchester City, Micah Richards akitoa matarajio yake kwa winga wa Liverpool, Mohamed Salah**



"Siku zote tunalia na maamuzi ya waamuzi, leo (Jumanne iliyopita), mwamuzi amewaongezea muda zaidi KMC na wakasawazisha bao, hii si sawa kabisa, waamuzi wanaua soka la Tanzania. Kwa maamuzi haya, kuna siku anaweza kutokea mtu akiwa na hasira na akafanya jambo la hatari sana. Kwa nini kila siku tunalia na waamuzi lakini hakuna hatua zinazochukuliwa?" **Msemaji wa Ruvu Shooting, Masau Bwire**



"Ninamkosa ('I miss') Lautaro Martinez, naweza kufia uwanjani kwa ajili yake tangu siku ya kwanza nilipokutana naye. Lautaro Martinez anakuja hapa kuwa nami Chelsea siku zijazo? Hapana... Lautaro, unaweza kubaki Milan, nitarejea huko (anacheka)," **Mshambuliaji wa Chelsea, Romelu Lukaku akielezea nia yake tena ya kutaka kurudi Inter Milan kucheza na Martinez.**



Nipashe
# Spotika


Kikosi cha ASEC Mimosas ya Ivory Coast kitakachoivaa Simba Kombe la Shirikisho Afrika. **PICHA: MAKTABA**

# WAJUE WAPINZANI WA SIMBA CAF NDANI NJE

**Na Adam Fungamwango**

JUMANNE iliyopita Shirikisho la Soka Afrika (CAF) lilichezesha droo ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Afrika hatua ya makundi ambayo yataanza kutimua vumbi Februari 11, mwaka huu.

Macho na masikio ya Watanzania wengi yalikuwa kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho ambapo wawakilishi pekee wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa, Simba, wapo.

Simba ambayo ilitolewa na Jwaneng Galaxy ya Botswana kwenye Ligi ya Mabingwa na kuangukia kwenye Shirikisho, ikifanikiwa kuitoa Red Arrows ya Zambia kwa jumla ya mabao 4-2, ikishinda 3-0 nyumbani na kuchapwa mabao 2-1 ugenini, ilipangwa Kundi D pamoja na ASEC Mimosas ya Ivory Coast, RS Berkane ya Morocco na USGN ya Niger.

Ni timu ambazo Watanzania wengi wanatamani kuzijua ubora wao ndani na nje kiundani, bila kuchelewesha mambo, hapa tunakudadavulia...

### RS BERKANE - MOROCCO

Ndiyo timu inayotabiriwa kuongoza kundi hilo kama siyo Simba. RS Berkane na Simba ndiyo zimetabiriwa na hata makocha mbalimbali na wageni waliohudhuria hafla ya droo hiyo nchini Misri.

Ndiyo timu pekee kwenye kundi hili iliyoanza moja kwa moja kwenye michuano hii, yaani haijatokea kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

Jina kamili la timu hiyo ni Renaissance Sportive de Berkane yenye maskani yake nchini Morocco ikianzishwa mwaka 1938, miaka miwili baada ya Simba.

Ni timu tishio si kwenye kundi tu, bali kwenye michuano yenye, kwani msimu wa 2019/20 ilitwaa kombe hilo shirikisho, na msimu kabla ya huo yaani 2018/19 ilifika fainali.

Ikumbukwe timu hii ndiyo anayeichezea Clatous Chama ambaye aliuzwa na Simba kwenye klabu hiyo mwanzoni mwa msimu huu, lakini winga wa zamani wa Yanga Tuisila Kisinda ni mmoja wa wachezaji wa timu hiyo.

Ilianza michuano hii kwa kuiondoa Ben Guerdane kwa jumla ya mabao 5-0, ikishinda 1-0 ugenini mabao 4-0 nyumbani raundi ya kwanza, huku ya pili ikikipiga na APR ya Rwanda, na kutoka suluhu ugenini kisha nyumbani kushinda 2-1, huku kutinga hatua ya makundi. Ikumbukwe RS Berkane ilianzia moja kwa moja raundi ya awali.

Kwa sasa inashika nafasi ya sita kwenye Ligi Kuu nchini humo ikiwa na pointi 20 kwa mechi 14 ilizocheza.

### USGN - NIGER

Ni timu ngeni masikioni mwa mashabiki wengi wa soka nchini Tanzania. Haipewi sana nafasi ya kusonga mbele, ingawa kwenye soka lolote linaweza kutokea.

Jina kamili la timu hiyo ni Union Spotive de la Gendarmerie Nationale na ina maskani yake jijini Niamey, nchini Niger.

Haina mafanikio makubwa sana kwenye soka la nchini humo, ingawa imetwaa ubingwa msimu wa 2021, pamoja na Kombe la Chama cha Soka nchini humo. Kwa misimu miwili ikitolewa mapema kwenye Ligi ya Mabingwa, kabla ya msimu huu kutolewa raundi ya kwanza na kuangukia hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho.

Ilianza kucheza kwenye Ligi ya Mabingwa tangu hatua za awali, ikiitoa Le Messeger Ngozi ya Burundi kwa jumla ya mabao 2-1, sare ya bao 1-1 ugenini na ushindi wa 1-0 nyumbani.

Ilikula kisago cha jumla ya mabao 7-1 dhidi ya Al Ahly ya Misri baada ya kutoka sare ya bao 1-1 nyumbani, kabla ya kupokea kichapo cha mabao 6-1 ugenini na kuangukia kwenye Kombe la Shirikisho ambako iliisukumiza nje Motema Pembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo kwenye mechi ya mtoano kwa jumla ya mabao 2-1, ikishinda 2-0 nyumbani na kupoteza kwa bao 1-0 ugenini.

Timu hii inashika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu nchini Niger, ikicheza mechi 11 na pointi zake 20.

### ASEC MIMOSAS

Simba itaanzia nyumbani kwenye mechi hizo za makundi dhidi ya Asec Mimosas Februari 13 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Ni timu ambayo ilicheza nayo mara mbili kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi mwaka 2003 mara ya kwanza ilikuwa Dar es Salaam kwenye Uwanja wa Taifa (sasa Uhuru), Agosti 24 mwaka huo, Simba ikishinda bao 1-0 lililofungwa na Ulimboka Mwakingwe, na mechi iliyochezwa nchini Ivory Coast, Oktoba 5, Simba ilikubali kichapo cha mabao 4-3 na kushindwa kusonga mbele kwenye hatua ya robo fainali baada ya kushika nafasi ya tatu kwenye Kundi A.


Imewahi kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Afrika mwaka 1998 na Super Cup mwaka 1999, pia ni timu ambayo mara kwa mara inaishi kwenye hatua za makundi ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho, huku hatua za robo na nusu fainali, ikiwa ni kawaida kwa timu hiyo kufika.

Ilianza kwenye Ligi ya Mabingwa kwenye hatua za awali tofauti na Simba, iliifunga Teungueth ya Senegal mabao 2-0 ikishinda bao 1-0 nyumbani na ugenini na kwenye raundi ya kwanza ikatolewa na CR Belouizdad ya Algeria kwa tofauti ya bao la ugenini kama ilivyokuwa Simba dhidi ya Jwaneng Galaxy. Ilishinda mabao 3-1 nyumbani, lakini ikachapwa mabao 2-0 ugenini ikawa 3-3, hivyo wapinzani wao hao wakapita kwa faida ya bao la ugenini na kuangukia Kombe la Shirikisho.

Kwenye mechi ya mtoano ilicheza dhidi ya Interclube ya Angola, ikashinda jumla ya mabao 5-3, ikishinda 2-0 nyumbani na 3-2 ugenini. Inaongoza ligi nchini kwao kwa kucheza mechi sita na imeshinda zote ikiwa na pointi 18.

Ilianzishwa mwaka 1948 na kubatizwa jina la The Association Spotive, des Employes de Commerce Mimosas, na hicho kikiwa kirefu cha ASEC.

### JE, WAJUA?



KIUNGO wa Simba, Rally Bwalya anakuwa mchezaji wa kwanza Ligi Kuu Bara tangu kuanza kwa mwaka huu kukosa penalti wakati timu yake pia ikiwa ya kwanza kuzawadia tuta kwa mwaka huu wa 2022. Hiyo ilitokea katika mechi dhidi ya Azam FC, Jumamosi.





Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano Mkoa wa Dodoma, Askofu Dk. Evance Chande (kushoto), akishirikiana na baadhi ya wachungaji na wainjilisti kuliombea taifa pamoja na viongozi walioko madarakani katika kuukaribisha Mwaka Mpya wa 2022, ibada iliyofanyika Kanisa la EAGT Ipagala, jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Serikali yasitisha uchimbaji madini ya nikeli

**Na Paul Mabeja,** CHAMWINO

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, amesitisha shughuli za uchimbaji wa madini ya nikeli katika eneo la mlima Yobo, wilayani Chamwino, kutokana na kutokidhi Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004.

Jafo alitoa agizo hilo juzi wakati wa ziara ya kikazi ya kukagua shughuli za mazingira katika maeneo ya wachimbaji wilayani humo.

Aidha, Waziri Jafo alimtaka mwekezaji kuusajili mradi huo katika ofisi za Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Kanda ya Kati ili wataalamu wajiridhishe kuhusu athari za mazingira katika eneo hilo.

"Hawa watu huko chini wataathirika na athari zinazoweza kutokea kutokana na uchimbaji huu usiofuata matakwa ya sheria na baadaye watakuja kuilaumu serikali kwa hiyo namwagiza aanze mara moja mchakato wa kupata cheti cha athari kwa mazingira (EIA)," alisema Jafo.

Alisema pamoja na kuwa wachimbaji wengi wanadai wana mpango kazi wa kulinda mazingira, lakini hauwezi kukidhi matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 na wanawajibika kupata EIA.

Kadhalika, alikiri nchi inajenga uchumi hususani katika sekta ya uchimbaji wa madini mbalimbali nchini, lakini ni lazima uendane na uhifadhi wa mazingira.

Katika hatua nyingine, waziri huyo akiwa wilayani humo alifanya ziara katika eneo linalochimbwa madini aina ya graphite, Kijiji cha Itiso na kubaini uchimbaji wa mashimo usiofuata taratibu.

Kutokana na hali hiyo alitoa miezi sita kwa Kampuni ya China Dragon inayofanya shughuli hizo hapo kuhakikisha wanakarabati eneo hilo ikiwamo kufukia mashimo hayo ili kukidhi matakwa ya mazingira.

Pia alitoa mwezi mmoja kwa kampuni kuja na mpango kazi wa namna gani watatekeleza maelezo hayo huku akiiagiza NEMC Kanda ya Kati kumpa taarifa ya utekelezaji wa agizo ndani ya kipindi hicho.

# TCDC Saccos yaja kivingine kuongeza mapato

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHAMA cha Ushirika wa Akiba na Mikopo (TCDC Saccos Limited), kimejipanga kuanzisha miradi mbalimbali ikiwamo uwakala wa huduma za kifedha kwa mitandao ya simu na benki ili kuongeza mapato ya chama na kujenga mtaji wa ndani.

Mwenyekiti wa Chama hicho, Aron Ibrahim, aliyasema hayo juzi kwenye mkutano mkuu wa chama hicho uliofanyika jijini hapa.

Alisema mkutano umeshauri kuwa Bodi ya Uongozi kuomba kibali kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika ili aruhusu kuendesha biashara ya uwakala wa mitandao ya simu pamoja na benki.

Vile vile, alisema chama kitaendelea kuhamasisha watumishi kujiunga na SACCOS hususan wa mikoani na wilayani, kuendelea kufuatilia na kutoa hamasa kwa wanachama kumaliza kulipa hisa na kuendelea kuweka akiba kila mwezi.

Pia alisema TCDC SACCOS, itaendelea kushirikiana na mwajiri kudhibiti wanachama wanaochelewesha marejesho ya mikopo.

Awali, akitoa taarifa ya ukaguzi, Mkaguzi kutoka Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO), Dora Meka, alisema hesabu za chama zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha unaoishia Desemba 31, mwaka 2019, zimezingatia viwango vya ukaguzi.

"Katika ukaguzi wa chama kwa mwaka 2019, chama hakikupata hoja yoyote kwa kuwa zilizojitokeza kwa miaka miwili ya nyuma mwaka 2017 na mwaka 2018 ambapo ilikuwa hoja ya kutumia 'cash basis' badala ya 'accrual basis', kamati ya usimamizi kutotekeleza majukumu yake, hoja hizi zilifanyiwa kazi kipindi cha ukaguzi wa mwaka 2019.

"Tunaipongeza Bodi ya TCDC SACCOS kwa usimamizi mzuri," alisema.

# Askofu Chande awageukia viongozi wa dini

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Maridhiano mkoani Dodoma, Askofu Dk. Evance Chande, amewataka viongozi wa madhehebu ya dini kutokuwa mahodari wa kuilaumu na kuinyooshea kidole serikali badala yake wawe wa kwanza kuiombea.

Vile vile, Dk. Chande, aliwataka viongozi hao wa kidini kuhakikisha wanajiepusha kwenye malumbano yasiyokuwa na tija, kwa kuwa yanaweza kuwa vichocheo vya kuhatarisha amani na utulivu uliopo uliozoeleka na Watanzania walio wengi kuishi kwa amani.

Alisema hayo kupitia mahubiri yake aliyotoa kwenye ibada maalumu ya kuukaribisha mwaka mpya wa 2022 iliyoambatana na maombi kwa ajili ya kuliombea taifa na viongozi wake akiwamo Rais, Makamu Rais, Waziri Mkuu, mawaziri, wakuu wa mikoa na wilaya iliyofanyika kanisa la EAGT, Ipagala.

Alisema viongozi wa dini wamepewa jukumu la kuombea amani, utulivu na umoja, na si kujiingiza kwenye malumbano yasiyo na tija.

Alisema kuwa bado kuna baadhi ya viongozi wa dini wameshindwa kusimama kwenye nafasi zao za kidini, badala yake wamejiingiza kwenye malumbano ya kuilaumu na kuinyooshea vidole serikali wakati hawastahili kufanya hivyo.

"Majukumu ya viongozi wa dini ni kuwaombea viongozi hao waliowekwa madarakani, kuombea amani na mahitaji mbalimbali yanayowagusa Watanzania kiroho na kimwili na kuonya pale panapostahili, na si vinginevyo.

"Hivyo niwaombe viongozi wenzangu tujiepushe kwenye hayo malumbano yasiokuwa na tija, bali tuwe mstari wa mbele kuhakikisha dua na sala zinadumu katika maisha ya kila Mtanzania ndani ya nchi yetu," alisema.

Hata hivyo, Dk. Chande aliwataka wafanyakazi katika sekta mbalimbali kufanya kazi kwa bidii na kwa malengo ya kuliletea faida taifa pamoja na wao huku wakitakiwa kutojilimbikizia mali kwa faida yao binafsi ikiwamo kughushi nyaraka za kujipatia fedha na mali.

Alisema ufanyaji kazi zao kwa bidii na uaminifu ndiyo nchi inavyoweza kuwa na maendeleo na kukua kwa uchumi, wanatakiwa kujituma huku wakiibua mbinu mbalimbali kwa lengo la kuongeza kipato zaidi.

Katika ibada hiyo ya maombi maalumu pia waumini waliombea mvua, makundi ya vijana na watoto ili wawe na maadili yakiroho, wakulima, wafanyabiashara, familia zenye ndoa na wimbi la nne la virusi vya corona ili litoweke na kutokomea nchini.



## Hospitali Busokelo yapigwa jeki mashuka

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

UMOJA wa Wanarungwe waishio maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi, wametoa msaada wa mashuka 50 katika Hospitali ya Halmashauri ya Busokelo, mkoani Mbeya ili kukidhi mahitaji ya wagonjwa.

Wakikabidhi msaada huo juzi, Mwenyekiti wa Asasi isiyokuwa ya kiserikali (Rungwe Yetu), Kenny Lawrence, alisema, unapofika mwezi Desemba kila mwaka hufanya mkutano mkuu wa mwaka kujadili maendeleo ya Wilaya ya Rungwe.

Alisema katika kuisaidia jamii ya Rungwe waneendelea kutoa misaada ya vitu mbalimbali ikiwamo mashuka hospitali na matangi ya maji yenye ujazo wa maji lita 5000 kwa soko la Kiwira na Tandale ili yaweze kuwasaidia wananchi wanaofanya biashara mbalimbali katika maeneo la Kiwira.

"Sisi kwa kila mwaka huwa tuna utaratibu wa kujitoa kwa wana Rungwe pamoja na kufanya mkutano mkuu kwa ajili ya kujadili masuala ya kimaendeleo yanayohusu Rungwe yetu na tunafanya hivi kuweka alama ili ndugu zetu walioko nje ya nchi waweze kurudi nyumbani na tuweze kushirikiana kwa pamoja na kutatua vikwazo mbalimbali," alisema Lawrence. Akipokea msaada huo wa mashuka, Kaimu Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Busokelo, Dk. Mayunga Kuyeyema, alishukuru kwa msaada huo ambao utatoa huduma za matibabu kwa ufanisi.

Aliwaomba wadau wengine kuisaidia hospitali hiyo mahitaji vifaa tiba na huduma nyingine za kitabibu ili kuwahudumia wagonjwa kwa ufanisi zaidi.

# Wanakyela wasaidia ujenzi jengo la wazazi

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

SHILINGI milioni 10, zilizotolewa na kikundi cha watu wa Kyela waishio maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi (IBHASA Group), kimesaidia ujenzi wa jengo na wazazi katika Hospitali ya Wilaya ya Kyela, mkoani Mbeya.

Kikundi cha IBHASA kinachounganisha Wanakyela waishio maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi kilianzishwa kwa lengo la kusaidia sekta ya afya, elimu, kukuza uchumi na kutembelea vivutio mbalimbali kila ifikapo mwisho wa mwaka na sasa ni mwaka wa tatu.

Mwenyekiti wa IBHASA, Eddo Mwamalala, akizungumza juzi wakati wa kukabidhi bima za afya kupitia CHIF iliyoboreshwa kwa kaya 100 zinazotoka katika mazingira magumu wakiwamo watoto na watu wenye ulemavu wilayani Kyela, alisema kiasi hicho cha fedha kimetokana na michango ya wanakikundi.

Alisema kiasi hicho kiliotolewa kuboresha huduma za mama na mtoto katika Hospitali ya Wilaya ya Kyela baada ya baadhi ya majengo kuungua na kusababisha msongamano wa wagonjwa.

"Kwa vile sisi ni jamii ya Kyela tuliamua kuweka utaratibu wa kila mwisho wa mwaka yaani Desemba kurudi nyumbani kuisaidia wilaya yetu katika nyanja za elimu na afya, lakini kuwaunga mkono wajasiriamali mbalimbali ili wakue kiuchumi na mambo mengi ambayo tumefanya kwa miaka mitatu hii tangu kuanzisha umoja wetu mwaka 2019," lengo letu ni kuhakikisha Kyela inakuwa ya mfano," alisema Mwamalala.

Akizungumza na Wanaibhasa, Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya ya Kyela, Dk. Mariam Ngwere, alisema, Sh. milioni 10 zilizotolewa na kikundi hicho zimesaidia ujenzi wa wadi ya wazazi ambayo imeanza kujengwa hivi sasa.

Alisema hadi sasa serikali imetoa Shilingi bilioni moja na litagharimu Sh. bilioni 3.8 litakalosaidiana kukabiliana msongamano wa wagonjwa.

"Tunahitaji kuwa na wazalendo wa namna hii ambao wanajitolea kuisaidia jamii yao, mchango wao umesaidia ujenzi wa jengo hili la wadi ya wazazi ambalo litakuwa la ghorofa moja, tunaomba wadau wengine watuunge mkono ili tukamilishe ujenzi huu ikiwamo nondo, saruji, kokoto, misumari au fedha," alisema Dk. Ngwere.

Aliongeza kuwa jengo hilo litakapokamilika litakuwa na vitanda 105 jambo alisema litasaidia kuhudumia wajawazito wengi kuliko ilivyo sasa ambao majengo hayatoshi.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Regina Kamala, aliwashukuru wanaibhasa kwa kujitoa kuisaidia jamii ya Kyela aliahaidi kuwapa ushirikiano wa hali na mali kufanikisha kuwahudumia wananchi.

Alitoa wito kwa Wanakyela wengine kujiunga na umoja huo au kujitoa kuisaidia jamii yao kwa madai kuwa jambo hilo ni jema na la baraka mbele za Mungu.



Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, Regina Kamala (katikati), akigawa kadi ya bima ya afya kupitia CHIF iliyoboreshwa kwa mtoto Bon Mwanyasi ambaye ni miongoni mwa wanufaika waliowezeshwa na kikundi cha IBHASA ambacho kimetoa kadi kwa kaya 100 zinazoishi mazingira magumu wilayani Kyela, mwishoni mwa wiki. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wakamilisha sekondari mpya kuokoa wanafunzi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mbeya kwa kushirikiana na wananchi vijiji vya Lusungo na Malowe wamekamilisha ujenzi wa sekondari mpya ya Malowe ili kuwasaidia watoto kuondokana na adha ya kutembea umbali mrefu.

Akizungumza na Nipashe juzi, Diwani wa Bonde la Songwe, Michael Ngailo, aliwashukuru wananchi kwa mwamko huo kuchangia ujenzi wa shule hiyo ambayo itakuwa msaada kwa watoto hususani wa kike kutimiza ndoto zao za elimu pamoja na kujiepusha na vitendo vya ukatili kama vile ubakaji na mimba.

Ngailo alisema kupitia vikao mbalimbali vya Baraza la Madiwani, aliiomba serikali kuisaidia kata yake hususani vijiji vya Lusungo na Malowe ambavyo jiografia yake si nzuri kujengwa sekondari ili kuwasaidia watoto kuondokana na adha ya kutembea umbali mrefu huku wakihatarisha usalama wao.

Alisema baada ya serikali kusikia kilio hicho walianza kuhamasisha wananchi kuchangia nguvu kazi zao huku nayo ikiendelea kutafuta fedha ili kuanza ujenzi wa sekondari mpya ya Malowe. "Nawapongeza sana wananchi wangu kwa kujitoa kukamilisha ujenzi wa sekondari hii, naamini wanafunzi wetu watasoma kwa raha na ndoto za maisha yao zitatimia kupitia elimu kwani kikwazo kikubwa tayari tumekiondoa, nawaomba tuendelee kujitoa zaidi ili kukamilisha miundombinu mingine," alisema Ngailo.

Miongoni mwa wananchi, Justa Elikaga, alisema wakati mwingine walilazimika kuwapangishia watoto wao nyumba ili kukaa karibu na maeneo ya shule kuliko kutembea umbali mrefu wa kilomita 12 kwenda shule. Alisema kutokana na ari waliyonayo waliamua kujenga vyumba vitatu vya madarasa huku serikali ikiwaunga mkono kukamilisha majengo hayo na huduma nyingine zinazohitajika.

Kwa upande wake, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Oran Njeza, aliwaahidi wananchi kuchangia fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vyoo ili shule zinapofunguliwa vianze kutumika.





# Shule iliyofutiwa usajili yawa kinara kufanya vizuri

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar imetangaza matokeo ya mtihani wa darasa la nne, sita na kidato cha pili kwa ufaulu kushuka kwa asilimia 2.55 ikilinganishwa na mwaka 2020 uliokuwa asilimia 81.40.

Katika matokeo hayo, Shule ya Eden ambayo imefutiwa usajili na Wizara ya Elimu mwishoni mwa mwaka jana imekuwa kinara kati ya shule 10 zilizofanya vizuri katika mitihani ya darasa la sita.

Shule hiyo imefutiwa usajili na kutoendelea kutoa elimu kutokana na kukiuka taratibu na sheria ikiwamo taratibu za uwekezaji na kushindwa kulipa kodi.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Ali Khamis Juma, alisema watahiniwa 52,290 wa darasa la nne walifanya mitihani yao na 41,231 wamefaulu huku wasichana wakiongoza kwa asilimia 42.78 na wavulana asilimia 36.07. Alisema wanafunzi 46,355 walifanya mitihani yao ya darasa la sita na watahiniwa 19,927 walifaulu, waliofaulu kwa kiwango cha D wataendelea na darasa la saba na waliofaulu kwa kiwango cha A, B, C ambao ni 213 watapangiwa katika madarasa ya vipawa maalum, 2,167 michepuo na 17,547 kidato cha kwanza sekondari ya kawaida.

Alisema ubora wa ufaulu kwa daraja la A, B na C kwa darasa la sita umeshuka kwa asilimia 4.08 ikilinganishwa na asilimia 47.07 ya mwaka 2020.

Kadhalika alisema kuwa Wilaya ya Micheweni Pemba, inaongoza kwa kufanya vizuri zaidi katika mitihani hiyo kwa asilimia 99.74, ikifuatiwa na Wilaya ya Mkoani yenye asilimia 99.60 na Wilaya ya Kusini Unguja imepata asilimia ndogo ya ufaulu ambayo ni 95.61.

Akitangaza matokeo ya kidato cha pili, alisema jumla ya watahiniwa 25,227 waliofanya mitihani hiyo, 31,955 wamefaulu na ufaulu huo umepanda kwa asilimia 14.25 ikilinganishwa na asilimia 12.96 mwaka 2020.

Alisema pia Wilaya ya Micheweni Pemba inaongoza kwa ufaulu wa kidato cha pili kwa kuwa na asilimia 86.31 na Wilaya ya Kusini Unguja imeshika mkia kwa kuwa na asilimia ndogo ya ufaulu wa asilimia 53.89.

Vile vile, wanafunzi 10 bora kitaifa wa kidato cha pili, Shule ya Fidelcastro Pemba imetoa wanafunzi tisa na Shule ya Lumbumba Unguja imetoa mwanafunzi mmoja.

Hata hivyo, alisema katika mitihani hiyo ya darasa la nne, sita na kidato cha pili hakukuwa na kesi yoyote ya udanganyifu na kuwapongeza wanafunzi waliofaulu huku akiwasisitiza kuongeza bidii kukuza uwezo wao wa kitaaluma kwa ajili ya kupata ufaulu mzuri zaidi katika mitihani ijayo.

"Pia niwapongeze walimu kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuwapatia wanafunzi taaluma na maadili mema mambo ambayo yatawasaidia wakati wa sasa na baadaye...pongezi kwa wazazi na walezi wa wanafunzi kwa kuwasimamia, kuwalea, kuwaongoza na kuwapatia watoto wao huduma za lazima ili kumudu masomo yao," alisema.




Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Mohammed Said, akifungua pazia kuashiria uwekaji wa jiwe la msingi katika kiwanda cha bomba za plastic cha Kasu kilichoko Maruhubi ikiwa ni maandalizi ya maadhimisho ya Miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waziri awaasa vijana watakaopata ajira

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohamed Said, amewataka vijana watakaobahatika kupata fursa za ajira katika kiwanda cha mabomba ya plastic (Kassu Industrial Ltd), kufanyakazi kwa bidii ili kupata mafanikio.

Aliyasema hayo wakati akiweka jiwe la msingi katika kiwanda hicho Maruhubi Mjini Unguja ikiwa ni shamrashamra za kutimiza miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964 viwanda vingi vilijengwa ili kuongeza ajira hasa kwa vijana.

Alisema viwanda hivyo vilifanyakazi kwa ufanisi mkubwa hadi pale palipotokea mabadiliko ya kiteknolojia ulimwenguni na viwanda hivyo vilishindwa kukabiliana na mabadiliko hayo na kuanza kushindwa kuzalisha kwa faida na kupelekea kufungwa kimoja baada ya kingine.

Waziri Simai alisema miongoni mwa viwanda vilivyoshamiri katika miaka hiyo katika eneo hilo ni kiwanda cha sigara (Tabia Njema), kiwanda cha ngozi na viatu (Mwendo), kiwanda cha maziwa na kiwanda cha chakula cha mifugo, pamoja na kiwanda cha nguo cha Cotex.

Alisema nchi zilizoendelea zimekuwa zikifanya jitihada mbalimbali ambazo zinaweza kupatikana kadri sekta inapoimarika ikiwamo fursa za ajira kwa wananchi, kuchangia pato la taifa kupitia kodi na tozo mbalimali ili kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje.

Akitoa maelezo mafupi kuhusu ujenzi huo, Katibu Mkuu Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Dk. Islam Seif, alisema mradi huo umeanza mwaka 2016 na wawekezaji wazalendo na kuunga mkono azma ya Serikali ya Zanzibar.

Alisema kuwa wanatarajia kuwa wanufaika wa kiwanda hicho ni wananchi wazalendo na kitakapokamilika kina uwezo wa kuzalisha na kuuzwa katika masoko ya Zanzibar na nchi jirani.

Alisema kiwanda hicho kinatumia vitu vya plastiki hivyo itarahisisha kuondosha taka za plastiki na kuzitumia kama malighafi.

Kwa upande wake mwekezaji wa kiwanda hicho, Hussein Kassu, alisema kiwanda hicho kimeanzishwa ni baada ya kuona kuna haja ya kuzalisha bidhaa hizo ili kurahisisha upatikanaji wa soko nchini.

Alisema katika kuleta jitihada za kuwapatia ajira vijana, wameamua kujenga kiwanda hicho na ni salama kwa wananchi na mazingira yaliyopo kwa sababu hakizalishi kemikali yoyote ya inayochafua mazingira.

Alisema changamoto inayowakabili ni gharama kubwa za tozo za na kukatika kwa umeme mara kwa mara jambo ambalo linawatia hofu ya kupanda kwa gharama zaidi baada ya kuanza kufanya kazi kwa kiwanda hicho.

## Wanadiaspora watakiwa kuwa mabalozi wa uwekezaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANADIASPORA wanaoishi katika mataifa mbalimbali ulimwenguni wametakiwa kuwa mabalozi wazuri wa kuzitangaza fursa za uwekezaji zinazopatikana Zanzibar ili kukuza uwekezaji na maendeleo nchini.

Hayo yalielezwa juzi na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Dk. Habiba Omar, katika mkutano wa Wanadiaspora, taasisi za umma na binafsi uliolenga kujadili na kuandaa mikakati ya ushirikishwaji wa Wanadiaspora, katika fursa za uwekezaji na biashara Zanzibar.

Alisema endapo wawekezaji kutoka mataifa mbalimbali ulimwenguni watawekeza Zanzibar katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii, wataisaidia serikali kutekeleza mipango ya maendeleo. Alisema kuwa, Zanzibar zipo fursa nyingi za uwekezaji katika sekta tofauti ikiwamo uchumi wa bluu, uvuvi wa bahari kuu, mwani pamoja bandari na kuwataka wanadiaspora kuwa mabalozi wazuri wa kuzitangaza fursa hizo.

"Hata kama mnaishi nje na nyumbani bado, mnahitajika katika kuungana na wananchi na serikali jitihada za kuleta maendeleo kupitia uwekezaji kwa kuwahamasisha wananchi wetu wanaoishi mataifa mbalimbali waje wawekeze nyumbani," alisema Katibu Mkuu.

Vile vile, alisema ushirikishwaji wa wandiaspora katika makongamano mbalimbali ya maendeleo umesaidia kwa kiasi kikubwa kuvuta uwekezaji na kuzitangaza fursa mbalimbali za kiuchumi zilizopo nchini.

Naye Mkurugenzi wa Diaspora, Adila Hilali Vuai, alisema wanadiaspora wamekuwa wazalendo kwa nchi yao kwa kutekeleza sera na ajenda mbalimbali za kiuchumi na maendeleo ili kuijenga Tanzania.

Alisema, wanadiaspora wanaendelea kushirikiana na serikali katika kushiriki na kutekeleza miradi ya maendeleo inayotekelezwa nchini.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Umoja wa Miradi ya Wawekezaji (TDH), Nassor Ali Basalama, alisema sera nzuri ya uwekezaji iliyowekwa Zanzibar pamoja na mazingira mazuri ya uwekezaji yameuhamasisha umoja huo kuweka nia ya kuwekeza Zanzibar katika sekta mbalimbali ikiwamo sekta ya kilimo.

Alisema kuwa, umoja huo umeamua kwa makusudi kufika Zanzibar ili kutizama na kukagua maeneo yote yenye mazingira ya uwekezaji kwa lengo la kuwekeza visiwani hapa.

Akiwasilisha mada kuhusu fursa za uwekezaji zinazopatikana Zanzibar, Ofisa kutoka Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), Khamis Dunia, alisema Zanzibar kuna fursa nyingi za uwekezaji ikiwamo visiwa vidogo vidogo, bandari pamoja uwapo wa mafuta na gesi na kuwataka wanadiaspora kuwekeza katika fursa hizo.

Alisema mamlaka inaendelea kutengeneza vivutio mbalimbali vya uwekezaji ili kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji pamoja na kurahisisha utoaji wa huduma kwa wawekezaji.

Akiwasilisha mada kuhusu fursa za uwekezaji katika uchumi wa bluu na uvuvi, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Uchumi wa Bluu na Uratibu, kutoka Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi, Hamad Bakari Hamad, alisema zipo fursa nyingi za uwekezaji katika uvuvi wa Bahari kuu kupitia meli za uvuvi na uwekezaji wa viwanda vya kusarifu samaki.

Alisema, serikali imeamua kuifanya Pemba kuwa eneo maalumu la uwekezaji, amewataka wanadiaspora kutembelea maeneo mbalimbali ya kisiwa hicho ili kuona fursa mbalimbali za kuwekeza. Ofisa Masoko kutoka Kamisheni ya Utalii, Khalfan Ali Mohammed, alisema sekta ya utalii ina maeneo mengi ya kuwekeza nchini, ikiwamo uwekezaji katika visiwa vidogo ikiwamo ujenzi wa hoteli.

# MATUKIO MBALIMBALI YA WIKI



Watoto wa Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara, wakisherehekea sikukuu ya Mwaka Mpya 2022 kwenye bwawa la kuogelea lililopo Mazubu Grand Hotel juzi. **PICHA: GIFT THADEY**



Diwani wa Kata ya Kigamboni, Dotto Msawa (kulia), akimkabidhi msaada wa magodoro Katibu wa Taasisi ya Kigamboni Community Centre (KCC), Kondo Rashid, kwa ajili ya kuwahudumia vijana walioathirika na dawa za kulevya, wilayani Kigamboni, mwishoni mwa wiki. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Fundi Seif Ali, akitengeneza matranka kwa ajili ya matumizi ya wanafunzi katika Soko la Vetenari jijini Dar es Salaam jana, tranka moja liliuzwa kwa Sh. 13,000 kwa bei ya jumla. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Mfanyabiashara wa samaki katika mwalo wa Kibirizi Manispaa ya Kigoma Ujiji, Juma Muheza, akionyesha samaki aina ya sangara aliyevuliwa katika Ziwa Tanganyika. **NA MPIGAPICHA WETU**



Wataalamu kutoka Chuo cha Ardhi Morogoro (ARIMO) wakiwa katika matayarisho ya awali ya kazi ya urasimishaji makazi holela katika Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya mwishoni mwa wiki. **NA MPIGAPICHA WETU**

## HABARI KIMATAIFA

# Ethiopia, Mali, Guinea zatolewa AGOA

**New York,** MAREKANI

ETHIOPIA, Mali na Guinea zimezuiwa kupata huduma ya kutotozwa ushuru kupitia mpango wa biashara wa AGOA ulio chini ya Marekani, kutekeleza agizo la Rais Joe Biden, kutokana na ukiukwaji wa haki za binadamu.

Mkataba uliopewa jina la Sheria ya Ukuaji wa Uchumi na Fursa Barani Afrika (AGOA), ulianza kufanya kazi mwaka 2000 chini ya utawala wa rais wa wakati huo wa Marekani, Bill Clinton, kuwezesha na kusimamia biashara kati ya Marekani na Afrika.

Mataifa yaliyomo kwenye mpango huo, yananufaika kibiashara nchini Marekani na kwa bidhaa ambazo zinatoka barani Afrika, ambazo huingia Marekani, bila kutozwa ushuru.

**Kufikia mwaka 2020, mataifa 38 yalikuwa tayari kwenye mfumo huo wa AGOA, kwa mujibu wa tovuti ya Mwakilishi wa Biashara wa Marekani.**

Haya yanajiri siku chache baada ya Rais Joe Biden kuzitishia nchi ambazo zina ukiukwaji wa haki za binadamu pamoja na zilizo na mapinduzi katika mataifa hayo.

Katika taarifa yake, Ofisi ya Mwakilishi wa Biashara wa Marekani, ilisema Marekani imeziondoa nchi hizo katika mpango wa AGOA, kutokana na hatua zilizochukuliwa na serikali zao ambazo zilikwenda kinyume na sheria za mpango huo.

"Marekani hivi leo (juzi) imeziondosha Ethiopia, Mali na Guinea kutoka kwenye programu ya biashara ya AGOA, kutokana na vitendo vya kila serikali kuvunja mkataba wa AGOA," ilisema Ofisi ya Mwakilishi wa Biashara wa Marekani, kwenye taarifa yake iliyotolewa Januari Mosi.

Hatua hiyo ya Marekani, inatishia sekta ya viwanda vya nguo nchini Ethiopia, ambayo husambaza bidhaa kwa kampuni za nguo za fasheni duniani na pia dhamira ya taifa hilo la Pembe ya Afrika, kuwa kituo kikuu cha utengenezaji bidhaa za viwandani.

Vile vile inaongeza mbinyo kwenye uchumi ambao tayari umeathirika kutokana na vita, Kaskazini mwa Ethiopia, janga la virusi vya corona na kupaa kwa bei ya bidhaa muhimu.

Novemba, mwaka jana, Rais Biden alionya kwamba Ethiopia ingeliondolewa kutoka kwenye mfumo wa AGOA kutokana na madai ya ukiukaji wa haki za binadamu katika eneo la Tigray, huku Mali na Guinea zikilengwa kutokana na mapinduzi ya hivi majuzi.

Chini ya makubaliano ya AGOA, maelfu ya bidhaa kutoka Afrika zinafaidika na punguzo la kodi kwa masharti kwamba, serikali za mataifa husika ziheshimu haki za binadamu, utawala bora na ulinzi wa wafanyakazi pamoja na kutoweka marufuku ya ushuru kwa bidhaa za Marekani, zinazoingia kwenye maeneo yao.

Kufikia mwaka 2020, mataifa 38 yalikuwa tayari kwenye mfumo huo wa AGOA, kwa mujibu wa tovuti ya Mwakilishi wa Biashara wa Marekani.

Mkataba huo, uliboreshwa mwaka 2015 na Baraza la Congress la Marekani, ambalo pia liliuongezea muda hadi mwaka 2025. **DW**

## Kasi 5G tishio kwa masafa ya ndege

**Washington,** MAREKANI

MAREKANI imetoa wito wa kutaka kucheleweshwa kwa shughuli ya usambazaji wa Mtandao wa Kasi ya '5G' kwenye simu za mkononi kutokana na uwezekano kuathiri usafiri wa anga.

Waziri wa Uchukuzi, Pete Buttigieg na Mkuu wa Usimamizi wa Anga (FAA), Steve Dickson, wametoa wito kwa waendeshaji wa mtandao wa AT&T na Verizon, kuahirisha kwa wiki mbili, uzinduzi wa mtandao huo uliopangwa kufanyika, keshokutwa.

FAA, inahofia teknolojia ya 5G inaweza kuingilia utendaji kazi wa vifaa fulani vya kielektroniki vya ndege, na kuongeza kuwa masafa yanayotumika na mtandao wa 5G nchini Marekani, ambayo kasi yake inayotumika inafanana na masafa ya altimita yanayotumika kwenye ndege. **DW**






Wazimamoto wakielekeza maji eneo la jengo la Bunge la Afrika Kusini, ambalo lilianza kuwaka moto jana asubuhi, mjini Cape Town. **PICHA: AP**

## Moto wazuka Bunge Afrika Kusini chanzo hakijabainika

**Cape Town,** AFRIKA KUSINI

JENGO la Bunge la Afrika Kusini, limewaka moto na kwamba chanzo cha moto huo bado hakijafahamika.

Moto huo umezuka chini ya saa 48, tangu mazishi ya kitaifa ya Askofu Desmond Tutu, kufanyika katika kanisa la St. George lililoko karibu na jengo hilo la bunge.

Waziri wa Ujenzi wa Umma na Miundombinu, Patricia De Lille, aliwaambia waandishi wa habari kwamba hakuna taarifa za majeruhi wala sababu ya moto kwenye jengo hilo.

Waziri De Lille, alisema moto huo kwenye jengo la Baraza la Kitaifa na Mikoa (NCOP), ulikuwa umedhibitiwa.

"Vyanzo vya habari vilisema kwamba moto huo ulianzia jengo la tatu kwenye bunge hilo, na kusambaa maeneo mengine," Jean-Pierre Smith, mjumbe wa kamati ya meya jiji la Cape Town, anayeshughulikia ulinzi na usalama, alisema.

"Moto umedhibitiwa upande mmoja na wazimamoto wanajaribu kudhibiti pia upande mwingine."

"Tunajaribu kila tuwezalo ili moto usisambae zaidi. Pia napenda kukishukuru kikosi cha zimamoto,"alisema De Lille.

Smith, alisema kamati imekwishabaini athari za awali kutokana na moto huo, ikiwamo nyufa kwenye kuta za jengo na kwamba wazimamoto wapatao 60 na magari ya zimamoto 12 kwenye eneo la tukio.

Moshi ulianza kuonekana kidogo kidogo kwenye jengo hilo, na eneo la kuingia lango kuu.

**REUTERS/SABC**

# MAKOCHA TIMU LIGI KUU Z'BAR WAPANIANA MAPINDUZI CUP

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya Namungo na Meli 4 City FC kukata utepe wa michuano ya Kombe la Mapinduzi 2022 jana, kinyang'anyiro hicho kitaendelea kutimua vumbi leo kwa kupigwa michezo miwili.

**Majira ya saa kumi Alasiri utapigwa mchezo kati ya Selem View dhidi ya Mlandege wakati saa mbili usiku ikipigwa mechi nyingine kati ya Taifa Jang'ombe na KMKM.**

Wakizungumza na waandishi wa habari jana, makocha wa timu hizo, kwa upande wa Kocha wa Selem View, Ali Kisaka, alisema wamejiandaa vizuri kuhakikisha wanafanya vizuri katika mchezo wao wa kwanza wa kombe hilo ambalo linafuatiliwa na mashabiki wengi ndani na nje ya Zanzibar.

Alisema anawaheshimu wapinzani wao Mlandege kwa kuwa wote wapo katika Ligi ya Zanzibar na haitakuwa kazi rahisi kwani tayari wameshasomana mbinu za uchezaji ingawa kila timu inaweza kuja na mbinu mpya itakayowapa alama tatu muhimu.

Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa Timu ya Mlandege, Jaala Abdallah Salum, alisema kikosi chake kimejiandaa kushinda na kurejesha hamasa kwa mashabiki wa timu hiyo.

Alisema licha ya kwamba katika mashindano haya watamkosa mshambuliaji wao, Abdulnasir Asaa, ambaye anauguza majeraha ya jicho baada ya kuumia katika michezo ya Ligi Kuu Zanzibar, lakini haitakuwa sababu kwa timu yao kukosa alama tatu.

Naye Kocha wa Timu ya Taifa Jang'ombe, Omar Khamis "Matu", alisema timu anayocheza nayo wameshakutana katika Ligi Kuu Zanzibar, hivyo kutakuwa na kazi kubwa ya kusaka alama tatu.

Alisema wapinzani wao, KMKM ni timu kubwa na inauzoefu katika michuano ya nje na ya ndani, hivyo dakika 90 ndizo zitakazoamua matokeo.

Kocha Ame Msimu wa timu ya KMKM yeye alisema kikosi chake kipo vizuri baada ya kuanza mapumziko ya Ligi Kuu, hivyo matarajio yake ya kuvuka katika hatua ya makundi watayafikia.

Aidha, alisema lengo si kushinda mchezo huo tu, bali ni kuhakikisha wanapambana kulibakisha kombe hilo Zanzibar ambalo kwa sasa linaloshikiliwa na Yanga ya Tanzania Bara.




Mkuu wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Halima Bulembo (mbele katikati), akiwa na baadhi ya watoto wenye uhitaji maalum walionyesha vipaji vyao katika Shindano la Miss Muheza kwa watu wenye ulemavu wa akili lililofanyika Ijumaa iliyopita na Mwajuma Salimu (aliyekaa) kutwaa taji hilo baada ya kuibuka mshindi huku akifuatiwa na Lidya Peter, Rehema Salehe na Mariam Joshua, ambao walipewa zawadi za mabegi. Wapili kulia ni Miss Kiziwi Afrika, Hadija Kanyama. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Yanga yathibitisha kumsajili Nkane

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE Klabu ya Yanga imemtambulisha rasmi straika Denis Nkane kuwa mchezaji wao ikimsajili kwa misimu miwili, alitokea Biashara United.

Kwenye mtandao rasmi wa instagram wa klabu hiyo umetoa picha ya mchezaji huyo na kumkaribisha kwenye maisha yake mapya.

Lilikuwa ni suala ya muda tu, kwani dalili zote zilionekana mchezaji huyo ambaye hucheza kama winga, kuwa maisha yake kwenye klabu ya Biashara United yanaelekea ukingoni na anaelekea Yanga.

Desemba 26, mwaka jana, wakati Yanga ikicheza dhidi ya Biashara United, mchezaji huyo alionekana jukwaani, lakini Desemba 30 ilipocheza dhidi ya Namungo alicheza, huku wachambuzi wa masuala ya michezo wakidai kuwa yalikuwa ni matayarisho ya kuelekea Jangwani.

Kusajiliwa kwa Nkane, kunaifanya klabu ya Yanga kufikisha wachezaji watatu wa Kitanzania mpaka sasa iliyowasajili katika dirisha hili dogo la Januari.

Tayari imewasajili kipa Aboutwalib Mshery kutoka Mtibwa Sugar, pia Salum Aboubakar Salum kutoka Azam FC.

Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema anahitaji tena wachezaji wawili, straika na beki ili kufunga usajili kipindi hiki cha dirisha dogo.

Mpaka sasa, Yanga haijasajili mchezaji yoyote kutoka nje ya nchi, ingawa muda wa usajili bado haujakamilika, ambapo dirisha linatarajiwa kufungwa Januari 15, mwaka huu.

# *Simba Queens, Ilala Queens vita vya mabao leo*

**Na Saada Akida**

NI vita nyingine kwenye Ligi Kuu ya Wanawake nchini, baada ya Simba Queens kueleza kuwa inachotaka ni kuendeleza ushindi kwa idadi kubwa ya mabao huku wapinzani wao, Ilala Queens wakidai safu yao ya ulinzi iko imara kupambana na 'Wekundu wa Msimbazi' hao katika mchezo huo utakaopigwa leo.

Katika mchezo huo, Ilala Queens watakuwa wenyeji wa mechi hiyo wakati wakiwakaribisha mabingwa watetezi wa ligi hiyo, Simba Queens katika dimba la Karume, Ilala liliopo Makao Makuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

Timu hizo zinashuka dimbani huku Ilala Queens ikiwa nafasi 11, ya pili kutoka mkiani baada ya kupoteza michezo yake miwili ya mwanzo wakati Simba Queens yenyewe imetoka kushinda kwa kishindo baada ya kutupia mabao 23 katika michezo yake miwili ya mwanzo, hivyo kukaa kileleni mwa msimamo wa hiyo inayodhaminiwa na Serengeti Lite.

Simba Queens wameanza vizuri msimu baada ya kuichapa Ruvuma Queens mabao 15-0 na kisha kuipa kichapo kizito Oysterbay Queens cha mabao 8-0, mechi zote zikipigwa Uwanja wa Mo Simba Arena, Bunju nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam.

Kutokana na idadi hiyo ya mabao waliyoyapata katika michezo hiyo miwili, Kocha Mkuu wa Simba, Sebastiana Nkoma, aliambia Nipashe kuwa anaiheshimu ligi na kila timu, lakini mipango yake ni kuhakikisha wanapambana kutafuta pointi tatu na kuwa makini kuhakikisha hawapotezi nafasi zao.

Alisema anawafundisha wachezaji wake kutumia vizuri nafasi wanazozitengeneza na kuhakikisha wanaendelea kufunga idadi kubwa ya mabao kila mechi.

"Nina waheshimu Ilala Queens, lakini hatutaingia kwa kuwadharau kwa sababu tumejianda vizuri kwa ajili ya kuhakikisha tunaenda kutafuta pointia tatu na tukipata nafasi ya kufunga idadi kubwa tutafunga ili kuendelea tulipoishia," alisema Nkoma.

Kocha Mkuu wa Ilala Queens, Antony Makunja, yeye alisema amekiandaa vizuri kikosi chake ikiwamo kuimarisha zaidi safu yake ya ulinzi ili kutokuwa miongoni mwa timu ambazo zitakazoingia katika orodha ya zilizofungwa mabao mengi na timu ya Simba.

"Mechi itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu sihitaji kuwa katika historia ya kwamba tumefungwa idadi kubwa ya mabao dhidi ya Simba Queens, lakini nahitaji kuwa timu ya kwanza kuwafunga mabingwa hao watetezi," alisema kocha huyo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### AUBAMEYANG KWA MKOPO

NEWCASTLE wamewasiliana na Arsenal na kuwasilisha pendekezo la kumtaka kwa mkopo mshambuliaji wa Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang, 32. ***(BBC Sport)***

### BEI YA NUNEZ YATAJWA

KLABU ya Newcastle wameambiwa wanatakiwa kutoa pauni milioni 50 kwa mshambuliaji wa Benfica na Uruguay, Darwin Nunez, 22. ***(Daily Mail)***

### TRIPPIER SUALA LA MUDA

MAOFISA wa Newcastle wana matumaini kwamba dili la kumnunua beki wa pembeni wa Atletico Madrid na England, Kieran Trippier,31, litakamilika siku chache zijazo. ***(Telegraph Sunday)***

### GALLAGHER AWANIWA PSG

KIUNGO wa kati wa Chelsea na England, Conor Gallagher, 21, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Crystal Palace, anawaniwa kwa pauni milioni 50 na Paris St-Germain. ***(Sun)***

### COUITINHO KUTUA EVERTON

KLABU ya Everton wamepewa ofa ya mchezaji wa Barcelona na Brazil, Philippe Coutinho, 29, huku kocha Rafael Benitez akitaka kumwongeza beki wa kulia wa Rangers na Scotland, Nathan Patterson, 20, kwenye kikosi chake. ***(Daily Mail)***

### LUIZ HUYOOO ARSENAL

ARSENAL wana nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Aston Villa na Brazil, Douglas Luiz, 23. ***(Sun Sunday)***

### GHAZI ATAKIWA WEST HAM

WINGA wa Aston Villa na Uholanzi, Anwar El Ghazi, 26, analengwa na West Ham Januari hii. ***(Football Insider)***

### TUANZEBE SAFI NAPOLI

NAPOLI wamekubali mkataba wa kumleta beki wa Manchester United, Axel Tuanzebe, 24, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Aston Villa. ***(Evening news Manchester)***

### BEEK MAMBO MAGUMU

MZOZO kati ya kiungo wa kati wa Uholanzi, Donny van de Beek, 24 na wakala wake wa zamani unamaanisha kuwa mchezaji huyo hana uwezekano wa kuondoka Manchester United Januari hii. ***(Sunday Mirror)***

### NKETIAH ATAKIWA LEVERKUSEN

KLABU ya Bayer Leverkusen wanataka kumsajili mshambuliaji wa Arsenal, Eddie Nketiah, 22, ambaye atakuwa mchezaji huru msimu wa majira ya joto. ***(Sun)***

### MUMIN ATAKIWA LEICESTER

LEICESTER City wana nia ya kumsajili beki wa Ghana, Abdul Mumin, 23, kutoka Vitoria Guimaraes ya Ureno. ***(Sunday Mirror)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# XAVI AMTAKA DEMBELE KUSAINI MKATABA MPYA

**Sidhani kama atakuwa na furaha mahali pengine kuliko Barca, nilimwambia tunamhitaji, ni...**

**BARCELONA,** Hispania

XAVI amemsihi Ousmane Dembele "kufanya juhudi" baada ya mazungumzo ya mkataba mpya kati ya Mfaransa huyo na Barcelona kugonga kikwazo.

**Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, ameingia miezi sita ya mwisho ya mkataba wake katika klabu hiyo, ikimaanisha kuwa anaweza kuanza kuzungumza na klabu nyingine kuhusu uhamisho wa bure mwishoni mwa msimu huu.**

Uchezaji wa Dembele pale Barca umekuwa wa kusikitisha kwa kiasi kikubwa tangu ajiunge nayo akitokea Borussia Dortmund kwa kiasi cha Euro milioni 105 mwaka 2017, huku majeraha yakimfanya kucheza mechi 86 pekee za LaLiga kati ya 165.

Hata hivyo, tangu Xavi ateuliwe kama mbadala wa Ronald Koeman Novemba mwaka jana, kocha huyo mpya amekuwa akizungumzia mara kwa mara jinsi anavyovutiwa na Dembele, akimuunga mkono kuwa mchezaji bora zaidi duniani katika nafasi yake.

Xavi bado ana matumaini kutokana na uvumi unaosema Barca na wawakilishi wa mchezaji huyo walifikia kikwazo katika mazungumzo, ingawa anataka Dembele atekeleze wajibu wake pia kama anataka kubaki.

Alipoulizwa kuhusu "mvutano" uliojitokeza katika mazungumzo, Xavi aliwaambia waandishi wa habari: "Sijakatishwa tamaa. Ni mazungumzo.

"Mawakala ni wagumu. Barca tuna msimamo wazi na unaendelea, haujaisha. Nina matumaini na ninatumaini Ousmane atafanya juhudi.

"Natumaini anaweza kubaki kwa sababu ni mchezaji mwenye uwezo wa kuleta mabadiliko na anaweza kuwa mwanasoka bora katika nafasi yake. Ni fursa kwake na hawezi kuikosa.

"Sidhani kama atakuwa na furaha mahali pengine kuliko hapa. Barca ni klabu bora zaidi duniani, mradi wa michezo utakuwa muhimu zaidi kuliko (kipengele) cha kiuchumi, na nimemjulisha. Hiyo ni kwa nini nina matumaini.

"Kwa kawaida nilimwambia kwamba tunamhitaji. Ni mchezaji muhimu kwetu. Anajua kwamba mradi huo unamvutia sana. Suala la kiuchumi halinihusu."

CHEZA USHINDE KASINO

MECHI KALI
HOME
AWAY
MANCHESTER UTD
1.64 | 3.74 | 5.49
WOLVERHAMPTON

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom
m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# TUCHEL: CHELSEA HAIJAKATA TAMAA



**LONDON,** England

THOMAS Tuchel amesisitiza kuwa Chelsea haitakata tamaa kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England dhidi ya Manchester City, lakini amekubali kwamba timu yake lazima iwe na ukweli kuhusu matarajio yao.

City walianza kuongoza kwa pointi 11 dhidi ya Chelsea walioko nafasi ya pili kwenye kilele cha Ligi Kuu kwa ushindi mnono wa mabao 2-1 dhidi ya Arsenal katika Uwanja wa Emirates Jumamosi.

Ni mara mbili pekee katika historia ya mashindano ambapo timu ilikuwa na faida kubwa zaidi mwishoni mwa Siku ya Mwaka Mpya - Manchester United mnamo 1993-94 na City mnamo 2017-18 (zote alama 12).

Chelsea jana Jumapili walikuwa na nafasi ya kupunguza pengo wakati wakicheza na Liverpool, ambao wana pointi moja nyuma katika nafasi ya tatu wakiwa na mchezo mkononi. Mbio hizo za kukatisha tamaa zimeambatana na Chelsea kukosa wachezaji muhimu kutokana na virusi vya corona na majeraha, na Tuchel anaamini kuwa timu yake ingekuwa karibu na City kama wangekuwa na kikosi chote.

"Kwa wakati huu, hiyo ndiyo faida kuu," alisema alipoulizwa kwa nini pengo kati ya City ni kubwa sana.

"Jambo la pili ni kwamba wanachukua faida hizi - hawana kuchoka, wanajua nini inachukua ili kuzalisha misimu hii ya juu mara kwa mara.



# Saha ampigia chapuo Zida

**PARIS,** Ufaransa

LOUIS Saha ana ndoto za Manchester United kumteua Zinedine Zidane, lakini amesisitiza kuwa wachezaji wa klabu hiyo lazima wamheshimu kocha yeyote aliyepo iwapo wanataka kufanikiwa.

United hawakucheza vizuri katika kipindi cha kwanza cha msimu wa Ligi Kuu England, wakiwa katika nafasi ya saba chini ya Ralf Rangnick baada ya kutimuliwa kwa Ole Gunnar Solskjaer.

Kocha wa zamani wa RB Leipzig, Rangnick amesimamia ushindi mara tatu na sare katika michezo yake minne ya ufunguzi wa ligi, lakini anahudumu kwa muda hadi mwishoni mwa msimu.

United tayari wamethibitisha kutafuta mbadala wake wa muda mrefu mwishoni mwa msimu huu, ambaye bado anaweza kuwa kocha huyo wa Ujerumani, huku wengine kama Zidane na Mauricio Pochettin
ipendekezwa.

Saha aliunga
Mfaransa mwenza
dane, ambaye an
hana klabu tangu a
doka Real Madr
mwaka jana, huku
buliaji huyo wa
wa United akielez
ya uteuzi anaoami
klabu hiyo inahitaji

Aliiambia Stats P
"Ninahisi kama mtu
ambaye amethibitis
njia fulani kwa kiwa
lani, nadhani Poche
mmoja wao.

LIVE IN PLAY



# MKUDE AWABWAGA ONYANGO, INONGA MCHEZAJI BORA SIMBA



**Na Mwandishi Wetu**

KIUNGO wa Simba, Jonas Mkude ametangazwa mchezaji bora wa Desemba wa timu hiyo na kuzawadiwa kitita cha Sh. milioni mbili kutoka kwa wadhamini wa klabu hiyo, Emirate Aluminium ACP.

Mkude ameibuka mshindi baada ya kuwabwaga mabeki wawili wa kati wa timu hiyo, Joash Onyanga na Henock Inonga 'Varane' waliokuwa wakiwania tuzo hiyo kwa Desemba. Mbali ya Desemba kuonyesha kiwango cha juu, pia Mkude amecheza mechi nne kati ya tano na kuhusika katika mabao mawili kwa kutoa pasi za mwisho.

Katika kura zilizopigwa na mashabiki wa klabu hiyo, Mkude amepata kura 2,397 sawa na asilimia 43.93 ya kura zote huku Onyango akipata kura 2,393 (43.85%) na Inonga akiambulia kura 667 sawa na asilimia 12.22.

Tangu kuumia kwa Taddeo Lwanga, Mkude ndiye anayetawala kiungo cha ulinzi cha Simba akisaidiana na Sadio Kanoute, kwa pamoja wakionyesha uwezo mkubwa wakuwalinda mabeki wa timu hiyo.

Uwezo wao umechangia kwa kiasi kikubwa Simba kushika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 24, tano nyuma ya Yanga iliyopo kileleni lakini ikiwa mchezo mmoja mbele.

ne
no wak-
mkono
ake Zi-
mekuwa
alipoon-
id Mei
msham-
zamani
za aina
ni kuwa
.
Perform:
u yeyote
sha kwa
ango fu-
ettino ni



# DTB haikamatiki kileleni Championship

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya DTB imeendelea kutesa kileleni mwa msimamo wa Ligi ya Championship baada ya kuendeleza ushindi kwa kuichapa Pamba FC bao 1-0 katika mechi kali iliyopigwa Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza juzi.

Bao pekee la DTB, liliwekwa kimyani na kiungo Mghana, Nicholas Gyan katika dakika ya 57, ushindi ambao unaifanya DTB FC sasa kufikisha alama 33 kileleni ikiwa ni pointi nne zaidi dhidi ya timu inayoshika nafasi ya pili Ihefu SC, wakati huu zote zikiwa zimeshuka dimbani mara 13 hadi sasa.

Kipigo hicho kinazidi kuiweka Pamba katika hali ngumu kwenye ligi hiyo inayoshirikisha timu 16, kwani kinaifanya kushika nafasi ya tisa ikiwa na pointi 16.

Katika msimamo wa ligi hiyo, Kitayosce FC ipo nafasi ya tatu ikiwa na alama 25 ikifuatiwa na JKT Tanzania na Mashujaa FC ambazo kila moja ina pointi 22.

Gwambia FC ndiyo inayoburuza mkia ikiwa na alama nne baada ya mechi 12 ikifuatiwa na African Lyon yenye pointi sita, lakini yenyewe ikiwa imeshuka dimbani mara 13.


SPORTPESA APP

BET LEO UWE MILIONEA


PAKUA SASA

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 03 - JANUARI 2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 2675 | Havadar vs Nassaji Mazandaran | 2.54 | 2.88 | 2.78 |
| 14:30 | 4673 | Padideh Mashhad vs Sepahan Esfahan | 5.20 | 3.22 | 1.67 |
| 14:30 | 5258 | Aluminium Arak vs Esteghlal Tehran | 2.92 | 2.87 | 2.44 |
| 14:30 | 5405 | Naft Masjed Soleyman FC vs Gol Gohar | 3.04 | 2.89 | 2.35 |
| 14:30 | 5865 | MES Rafsanjan vs Sanat Naft Abadan | 2.02 | 2.95 | 3.77 |
| 16:00 | 4648 | US Biskra vs WA Tlemcen | 1.44 | 3.75 | 7.12 |
| 16:10 | 2251 | Al-Shamal vs Al Gharafa SC | 4.83 | 4.35 | 1.51 |
| 16:30 | 1360 | Foolad Khuzestan vs Peykan FC | 2.35 | 2.99 | 2.94 |
| 16:30 | 2126 | Zob Ahan vs Fajr Sepasi | 2.22 | 3.04 | 3.13 |
| 17:00 | 1107 | Delhi Dynamos FC vs Mumbai City FC | 4.05 | 3.95 | 1.67 |
| 18:00 | 1097 | Bognor Regis vs Merstham | 1.92 | 3.66 | 3.28 |
| 18:00 | 1109 | Biggleswade Town vs Bromsgrove Rovers | 2.34 | 3.56 | 2.55 |
| 18:00 | 1116 | Redditch United vs Banbury United | 5.60 | 4.34 | 1.45 |
| 18:00 | 1386 | Folkestone Invicta vs Leatherhead | 1.36 | 5.00 | 6.15 |
| 18:00 | 1420 | Brightlingsea Regent vs AFC Hornchurch | 4.17 | 4.26 | 1.60 |
| 18:00 | 1692 | Kingstonian vs Lewes | 2.24 | 3.81 | 2.56 |
| 18:00 | 2677 | Horsham vs Corinthian Casuals | 2.30 | 3.86 | 2.46 |
| 18:00 | 2783 | Wingate and Finchley vs East Thurrock | 2.03 | 3.72 | 2.95 |
| 18:00 | 3410 | Sitra Club vs Bahrain Club | 2.26 | 3.22 | 2.88 |
| 18:00 | 3726 | Ethnikos Achnas vs Doxa Katokopia | 2.23 | 3.37 | 3.07 |
| 18:00 | 3753 | Cray Wanderers vs Enfield Town | 3.37 | 3.95 | 1.82 |
| 18:00 | 4065 | Cambridge Utd vs Portsmouth | 3.58 | 3.28 | 2.02 |
| 18:00 | 4099 | Al Ittifaq Bhr vs Malkiya Club | 3.10 | 3.40 | 2.26 |
| 18:00 | 4255 | Bowers Pitsea vs Margate | 2.84 | 3.85 | 2.05 |
| 18:00 | 4555 | Potters Bar Town vs Bishop Stortford | 3.37 | 3.95 | 1.82 |
| 18:00 | 4610 | Hungerford Town vs Hampton and Richmond | 2.66 | 3.43 | 2.32 |
| 18:00 | 4663 | Cheshunt vs Haringey Borough | 1.64 | 4.03 | 4.13 |
| 18:00 | 4788 | Taunton Town vs Tiverton Town | 1.67 | 3.95 | 4.05 |
| 18:00 | 4823 | AL Ittihad Bhr vs Busaiteen | 2.23 | 3.50 | 3.05 |
| 18:00 | 5195 | Nottingham vs Barnsley | 1.72 | 3.44 | 4.81 |
| 18:00 | 5280 | Carshalton Athletic vs Worthing | 2.98 | 4.04 | 1.93 |
| 18:00 | 5661 | Stoke City vs Preston | 2.13 | 3.19 | 3.38 |
| 18:00 | 5759 | Reading vs Derby | 2.25 | 3.15 | 3.15 |
| 18:20 | 5050 | Al-Sailiya SC vs Al Sadd SC | 18.29 | 8.47 | 1.08 |
| 18:20 | 5627 | Al Ahli Doha SC vs Qatar SC | 3.37 | 3.28 | 2.01 |
| 20:00 | 2248 | Apollon Limassol vs AEL Limassol | 1.78 | 3.57 | 4.36 |
| 20:00 | 2808 | AS Ashdod vs Hapoel Petah Tikva | 2.16 | 3.22 | 3.37 |
| 20:00 | 2824 | USM Alger vs MC Magra | 1.36 | 4.05 | 8.49 |
| 20:00 | 4729 | Hapoel Kfar Saba vs Hapoel Ramat Gan | 2.17 | 3.26 | 3.31 |
| 20:00 | 5253 | Maccabi Bney Reine vs Hapoel Rishon Lezion | 1.78 | 3.57 | 4.36 |
| 20:30 | 5902 | Manchester Utd vs Wolverhampton | 1.64 | 3.74 | 5.49 |
| 21:00 | 4500 | Vilafranquense vs Casa Pia Atletico | 3.36 | 3.21 | 2.10 |
| 21:00 | 4779 | Villarreal vs Levante | 1.34 | 5.37 | 7.76 |
| 21:30 | 1443 | Maccabi Haifa vs Maccabi Tel Aviv | 1.54 | 3.86 | 5.20 |
| 22:45 | 5159 | Beaconsfield Sycob vs Metropolitan Police | 4.24 | 3.95 | 1.64 |
| 23:00 | 1127 | Alcorcon vs Malaga | 2.46 | 2.95 | 3.00 |
| 23:00 | 5654 | Osasuna vs Athletic Bilbao | 3.15 | 2.95 | 2.47 |
| 23:10 | 4481 | Vannes OC vs Paris St Germain | 34.13 | 9.86 | 1.06 |
| 23:15 | 5887 | Cadiz CF vs Sevilla FC | 4.50 | 3.30 | 1.87 |
| 23:15 | 5997 | Tondela vs Moreirense | 2.43 | 3.26 | 2.81 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Januari 3, 2022

Nipashe




Xavi amtaka Dembele kusaini mkataba mpya

UKURASA 21

UNAPITAJE SASA!...



Kiungo wa Simba, Rally Bwalya, akijaribu kupenya safu ya ulinzi ya Azam FC wakati wa mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi na Wekundu wa Msimbazi hao kushinda 2-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Nabi aahidi makubwa Yanga mwaka 2022

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amewaahidi wanachama na mashabiki wa timu hiyo, kuwa 2022 ni mwaka wao wa kufurahi kwa kuhakikisha anatengeneza kikosi bora na kucheza soka safi ili kufikia malengo ya kutwaa kila taji hususan ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Nabi alisema watakaporejea wakitoka katika mapumziko mafupi ya kupisha michuano ya Mapinduzi, atakuwa amewapa mbinu za kiufundi wachezaji wake ili kuzidi kuwafurahisha zaidi mashabiki wao kwa matokeo mazuri na mchezo wa kuvutia.

Alisema anapenda kutuma ujumbe kwa mashabiki na Watanzania wote kwa ujumla juu ya mwaka mpya 2022 na malengo yao yapo pale pale kuendelea kupata matokeo chanya kwa kila mechi na pia wachezaji kucheza kandanda safi la kuvutia.

"Malengo yetu yako pale pale, kikubwa tunawaahidi mashabiki wa Yanga kuwa mimi si mtu wa maneno, kazi inaendelea bila matatizo na bado tutaendelea kuwafurahisha na kucheza soka safi ambalo litatupa matokeo mazuri," alisema Nabi.

Yanga ipo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 29 tano mbele ya watani zao wa jadi, Simba walioko nafasi ya pili, lakini wakiwa mchezo mmoja nyuma.

# PABLO SASA KUGEUKIA DARASA PENALTI SIMBA

### Amtaja Morrison, Nyoni na Bwalya akitaka kutumia Mapinduzi Cup kumaliza...

**Na Saada Akida**

LICHA ya ushindi walioupata dhidi ya Azam FC kwenye Ligi Kuu Bara juzi, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco, amesikitishwa na kukosa umakini kwa wachezaji wake katika upigaji penalti pindi zinapotokea, jambo ambalo ameahidi sasa kulivalia njuga mazoezini.

**Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, Simba ikiwa mwenyeji licha ya kushinda 2-1, kiungo wake, Rally Bwalya alikosa penalti kipindi cha kwanza baada ya Pape Sakho kuchezewa madhambi ndani ya eneo la hatari.**

Akizungumza baada ya mechi hiyo ambayo Sadio Kanoute na Sakho waliipa Simba ushindi huo, Pablo alisema atakwenda kulifanyia kazi mapema tatizo hilo kwa kuhakikisha katika mapumziko haya mafupi kikosi chake kinakuwa imara na tishio katika michezo iliyopo mbele yao ikiwamo Kombe la Mapinduzi, Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la Shirikisho Afrika.

Alisema mechi ilikuwa ngumu na ilitawaliwa na mbinu nyingi kutoka kila upande, jambo ambalo aliwapongeza wachezaji wake kwa kuonyesha mchezo mzuri na kila mmoja kutekeleza majukumu yake na hatimaye kufikia malengo yao ya kupata pointi tatu.

Kocha huyo raia wa Hispania, alisema ilikuwa mechi nzuri ya kuvutia na walitawala sehemu kubwa, ingawa walishindwa kutumia vema nafasi nyingi ambazo kama wangezitumia vizuri zingewafanya kuibuka na ushindi mnono ikiwamo penalti waliyoikosa.

"Mechi ilikuwa ngumu na ilitawaliwa na mbinu zaidi, tulimiliki sehemu kubwa ya mchezo na tulipoteza nafasi za kufunga pamoja na penalti, hii ni penalti ya tatu tumekosa kwa wachezaji watatu tofauti.

"Ni kweli kuna changamoto kwenye upigaji wa penalti, alianza kukosa Erasto Nyoni akafuata Bernard Morrison na leo (juzi) Rally Bwalya, bado nina muda mfupi kikosini, hivyo tutaendelea kurekebisha na kuwajenga nyota wangu katika hali ya kujiamini," alisema Pablo.

Alisema ushindi na kiwango kilichoonyeshwa umeongeza hali ya kujiamini kuelekea katika michuano ya Kombe la Mapinduzi iliyoanza kutimua vumbi jana visiwani Zanzibar.

Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa Azam FC, Iddy Abubakari, alisema walifanya makosa na Simba kuyatumia kuwaadhibu hatimaye kuibuka na pointi muhimu na sasa wanarudi uwanjani kufanyia kazi pale walipokosea.

Iddy alisema hawakucheza mpira mzuri kama ilivyo kwa wapinzani wao, Simba ambao walikuwa makini kutumia makosa yao na kuibuka na ushindi huo wa maboa 2-1.

"Tumemaliza mchezo huu, tunarejea uwanjani kwa ajili ya kufanyia kazi madhaifu yetu kwa kipindi chote ambacho ligi itakuwa imesimama na kutumia Mapinduzi Cup kuwa sehemu ya kuona zaidi mapungufu yetu," alisema Iddy.

Wakati huo huo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugezi wa Simba, Salum Abdalla `Try Again' aliwaondoa hofu mashabiki na wanachama wa klabu hiyo kwa kueleza kuwa timu yao imezidi kuimarika na ana imani hivi karibuni wataonekana kila Luis Miqussione wengine.

"Kuhusu usajili, mashabiki wanatakiwa kutulia na hilo suala linafanyiwa kazi na kamati husika kwa kupitia ripoti ya Pablo ikiwamo kuimarisha nafasi ambazo ameziona zinamapungufu kwa ajili ya kuboresha timu kuelekea mechi zetu za ligi na michuano ya kimataifa," alisema Try Again.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >